# Nipashe

Jumanne Aprili 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580205

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Ofisa muuguzi adaiwa kuuawa na mpenzi, azikwa shimo la choo

UKURASA 2


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Viuatilifu vilivyo kitisho unai wa mkulima, maji
ELIMU
Corona inavyoliamsha taifa kuboresha Tehama shuleni

UKURASA 11

## UTEUZI CHADEMA

# Mdee, Mnyika, Kubenea wapata wapinzani 2020

**WANASIASA** 72 watia nia ya kuwania ubunge Dar ...*Endelea ukurasa 2*



Saed Kubenea

John Mnyika

Halima Mdee

## CAG AANIKA HASARA YA MABILIONI FEDHA TBA

UKURASA 3

## Wagonjwa wa corona wafikia 46

UK 2

### BAA LA CORONA



Unaweza kupunguza uwezekano wa kupata maambukizi au kusambaza ugonjwa wa Covid -19 kwa kuchukua tahadhari ya kukaa umbali wa mita moja (futi tatu) kati yako na mtu mwingine anayepiga chafya au kukohoa. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo






MICHEZO MIHAYO AWATAKA SIMBA KUZINDUKA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Mdee, Mnyika, Kubenea wapata wapinzani 2020

**Na Enock Charles**

JOTO la uchaguzi ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), limeanza kupanda baada ya wagombea zaidi ya 72 kujitokeza kuwania ubunge katika majimbo 10 ya uchaguzi ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na chombo kimojawapo cha habari nchini, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alisema chama hicho kimeshafunga pazia kwa watia nia wa ubunge na udiwani Machi 30, baada ya kufunguliwa tangu Januari 29, mwaka huu.

"Kwa mfano katika Mkoa wa Dar es Salaam katika majimbo 10 ya uchaguzi, kuna wagombea mbalimbali waliojitokeza zaidi ya 72, unaweza ukaona ni jinsi gani mwitikio umekuwa mkubwa, hakuna jimbo lenye wagombea chini ya watatu," alisema Mrema.

**WABUNGE MAARUFU WAPATA UPINZANI**

Aidha, alisema kuwa Mbunge wa Kigoma Mjini na Kiongozi Mkuu wa chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, amepata mpinzani ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Sabreena Sungura.

Mbunge wa Kibamba ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, amepata wapinzani wawili, ambao ni madiwani katika jimbo hilo.

Wengine ni Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), na Mbunge wa Ubungo, Saed Kubenea, ambao wamepata wapinzani zaidi ya mmoja, ambao wanataka kuwania ubunge kwenye nafasi hizo.

Mdee amepata wapinzani wawili, mmojawapo akiwa ni mwanachama wa Chadema, Joel Mwakalebela.

Katika jimbo la Ubungo, wamejitokeza watia nia sita akiwamo Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob, kuchuana na Kubenea.

Hata hivyo, baadhi ya wabunge hawakutia nia ya kugombea nafasi mbalimbali ambao ni Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini, Mbunge wa Moshi Mjini, Jaffar Michael, Mbunge wa Moshi Vijijini, Anthony Komu na Mbunge wa Bukoba Mjini, Wilfred Lwakatare.

Katika mchakato huo, wapo wabunge wanaotarajia kubadili majimbo ya kugombea, ambao ni Mbunge wa Momba, David Silinde, aliyetia nia katika jimbo la Tunduma ambalo kwa sasa linaongozwa na Frank Mwakajoka.

Katika Jimbo la Kinondoni, wamejitokeza watu wanne akiwamo Mbunge wa Viti Maalum, Suzan Lyimo na Diwani wa Kinondoni, Mustapha Muro, huku jimbo la Segerea wakijitokeza wagombea wanne, akiwamo Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema na madiwani wawili Patrick Asenga na Manase Mjema.

Baadhi ya viongozi walio katika nyadhifa mbalimbali katika chama hicho waliojitokeza kugombea katika majimbo ni Mwenyekiti wa chama hicho Kanda ya Victoria, Ezekiel Wenje, anayegombea jimbo la Nyamagana, Mwenyekiti wa Kanda ya Kusini, Selemani Mathew, anayegombea jimbo la Mtama, Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake (Bawacha), Grace Tendega, anayegombea jimbo la Kalenga

Wengine ni Patrick Sosopi (Isimani) ,Sophia Mwakagenda (Rungwe), Catherine Ruge (Serengeti), Joyce Sokombi (Musoma Mjini), Salome Makamba (Shinyanga Mjini), Grace Kiwelu (Vunjo) , Hemed Ali (Lindi Mjini), Yoseph Komba (Muheza), Tunza Malapo (Mtwara Mjini), Rebecca Mdogo (Arumeru Mashariki), Lucy Owenya (Moshi Vijijini) na Gimbi Masaba (Musoma Mjini).

Kwa pande wa nafasi ya urais, Mkurugenzi huyo wa Chadema, alisema hawajafungua milango, lakini kanuni zinaruhusu yeyote mwenye nia ya kugombea kiti hicho kumwandikia barua Katibu Mkuu wa chama hicho kuhusu nia yake.

# Wagonjwa wa corona wafikia 46

**Na Waandishi Wetu**

WAGONJWA wa virusi vya corona ndani ya siku mbili wameongezeka wengine 14 na kufanya jumla yao wanaougua hadi sasa kufikia 46 kutoka 32 walioripotiwa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika taarifa yake aliyoitoa jana jijini Dodoma, alisema kuwa wagonjwa hao wapya 14 wote ni Watanzania.

"Aprili 10, tulikuwa na wagonjwa 32, ambao wamethibitika kuwa na maambukizi ya corona na leo (jana), wagonjwa wengine 14 wamethibitika kuwa na corona, na kufanya jumla yao kufikia 46 kutoka 32," alisema.

Ummy alisema kati ya wagonjwa hao 14, waliopo Dar es Salaam ni 13 na mmoja yupo jijini Arusha.

"Wagonjwa wote wanaendelea na matibabu chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya. Ufuatiliaji wa watu waliokuwa karibu na wagonjwa unaendelea.

"Serikali inarudia tena kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbalimbali hususan kuepuka misongamano na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima."



Mwalimu Mselema Regina wa Shule ya Msingi Mbunze Halmashauri ya Ushetu akiomba kura ya uwakilishi wa walimu wa shule za msingi kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu wilaya ya Ushetu. **PICHA: SHABAN NJIA.**

**HALI ZANZIBAR**

Kwa u[ande wake, Zanzibar imesema wagonjwa 12 wamelazwa katika kituo maalumu cha wagonjwa wa corona kilichopo Kidimni wilaya ya kati Unguja baada ya watu watatu kubainika kuambukizwa ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, alisema jana kuwa, wagonjwa watatu wapya wameongezeka baada ya kuchunguzwa damu na kubainika kuambukizwa ugonjwa huo.

Aidha, alisema wagonjwa wawili ambao wamelazwa katika kituo hicho katika Wilaya ya kati Unguja wameruhusiwa, baada ya kupona na kwamba wametakiwa kujitenga kwa siku 14 nyumbani.

Alieleza kuwa, wagonjwa watatu wapya waliotambuliwa wote wanatoka ndani ya nchi.

Alimtaja mgonjwa wa kwanza ni mwanamke mwenye umri wa miaka (30), mkazi wa Mwanakwerekwe mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, wakati mgonjwa mwingine ni mwanamume mwenye umri wa miaka (22), mkazi wa Jang'ombe Unguja.

Mgonjwa mwingine aliyelazwa kwa mujibu wa Hamad Rashid, alitambuliwa kuwa ni mwanamume mwenye umri wa miaka (19), mkazi wa Bumbwisudi wilaya ya Magharibi Unguja.

Alieleza kwamba wizara imefungua kambi nyingine kwa ajili ya kulaza wagonjwa wa corona iliopo Shule ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) Mtoni Mjini Unguja kutokana na kuongezeka kwa wagonjwa.

"Napenda kutoa taarifa kwamba, tumefungua kambi nyingine kwa ajili ya kulaza wagonjwa wa corona iliopo Shule ya JKU Mtoni Unguja, na hiyo inatokana na kuongezeka kwa wagonjwa," alisema Hamad Rashid.

Alisema hadi kufikia Aprili 12, jumla ya watu 164 waliokutana na wagonjwa wa corona wanafuatiliwa mienendo yao kwa karibu zaidi, huku watu 232 waliotoka safarini nje ya nchi kwa sasa wamewekwa katika karantini, ambapo wengine 264 waliruhusiwa kutoka karantini baada ya kukaa kwa siku 14.

***Imeandikwa na Romana Mallya, DAR na Rahma Sileiman, ZANZIBAR***


IN THE DISTRICT COURT OF NYAMAGANA
AT MWANZA

PROBATE AND ADMINISTRATION OF ESTATES NUMBER 01 OF 2020

IN THE MATTER OF THE ESTATES OF THE LATE OSCAR LUTHER KAZAULA

AND

IN THE MATTER OF PETITION FOR PROBATE
BY
ESTHER MGORE MALONGA

NOTICE TO CREDITORS

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debt or liabilities affecting the estate of the above-named Oscar Luther Kazaula, deceased, who died at Bugando Hospital in Mwanza on the 25th day of May 2019 and probate of whose Will was granted to me by the court on the 30th day of March 2020; are hereby required to send in their claims to me within two months of sixty days from the date of the publication of this notice through the following address bellow. At expiration of the time stipulated above, I shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims which I shall have had notice.

ESTHER MGORE MALONGA
EXECUTOR
ADDRESS:
BUGUKU STREET MKOLANI, NYAMAGANA, MWANZA CITY.
PHONE NUMBER: 0754390070



KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**STEVEN ELIAS KIMILA**
ANATANGAZA
KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA IST YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 598 DPN.** KWAYOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI :
**KAH/ / TR /RB/ 2550/2020.**


# Ofisa muuguzi adaiwa kuuawa na mpenzi wake

**Na Francis Godwin, IRINGA**

OFISA muuguzi msaidizi wa Zahanati ya Nyenza Kata ya Magulilwa, wilaya ya Iringa, Rachel Mwella (32), mkazi wa kijiji hicho cha Nyenza, anadaiwa kuuawa na mpenzi wake na mwili kuzikwa kwenye shimo la choo.

Imedaiwa kuwa, baada ya kuzikwa, mtuhumiwa alipanda mgomba, na kwamba sababu za mauaji ni wivu wa kimapenzi.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alisema kuwa, alipokea taarifa ya mauwaji hayo juzi majira ya usiku na kwenda eneo la tukio kupata undani wa tukio hilo.

Kasesela alisema ofisa muuguzi huyo alianza kazi mwaka 2012 na kabla ya kuuawa, alikuwa amepotea nyumbani kwake kwa siku kadhaa, na wananchi waliamua kuanza kumtafuta bila mafanikio.

Kwa mujibu wa Kasesela, wakati wa msako, wananchi walilishtukia shimo, hivyo kuamua kulifukua shimo hilo, na ghafla walishangazwa kuona mahindi yamefyekwa na kuwapo kwa dalili za watu kufukia kitu na kupanda mgomba juu yake.

Alisema walipofukua chini ndipo walipokutana na nguo zake kabla ya kukutana na mwili, ambao ulikuwa unavuja damu.

Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kuwa lilitokea Aprili 10 majira ya alfajiri.

Kamanda Bwire alisema anayetuhumiwa kufanya mauaji hayo ni mpenzi wa muuguzi huyo.

Kamanda Bwire alisema sababu za kufanya hivyo zinatajwa kuwa ni wivu wa kimapenzi na kuwa Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka mtuhumiwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa kumfichua mtuhumiwa huyo.

Haya ni mauaji ya pili kutokea ndani siku tatu katika wilaya ya Iringa, ambapo unyama kama huo ulifanyika katika eneo la Kijiweni Manispaa ya iringa.

Katika tukio hilo, watu wasiojulikana walimuua kwa kumchinja shingo mhubiri wa injili, Raymond Mdota (46), akiwa katika huduma ya kuhubiri injili kwenye klabu cha pombe za kienyeji Kijiweni, na mwili wake kutupwa kwenye shamba la mahindi.

HABARI KITAIFA

# CAG aanika TBA ilivyotengeneza hasara ya mabilioni ya fedha

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Wakala wa Majengo (TBA) na kutaja sababu za kupata hasara ya mabilioni ya shilingi na baadhi ya miradi yake kuhamishiwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anasema TBA ni wakala wa serikali chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) ulioanzishwa kwa lengo la kutoa makazi bora kwa serikali na watumishi pamoja na kutoa ushauri katika masuala ya ujenzi kwa serikali.

Hata hivyo, CAG Kichere anasema udhaifu katika ujenzi wa majengo ya serikali, akitolea mfano makubaliano na TBA na taasisi nyingine za serikali kujenga majengo mapya ya ofisi katika Mkoa wa Dodoma (Mji Mkuu) ili kuwezesha uhamishaji wa shughuli za serikali.

Anasema kuwa katika ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo, alibaini udhaifu kadhaa ikiwa ni pamoja na usanifu na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Katika mradi huu nimebaini hasara ya kiasi cha Sh. 8,854,624,244.25 (bilioni 8.855) iliyotokana na kukataliwa kwa madai ya ongezeko la kazi (mabadiliko Na. 1&2).

"Madai haya yalikataliwa kutokana na mkandarasi (TBA) kutekeleza kazi za ziada bila kupata idhini ya mwajiri (NEC) kinyume cha Kifungu kidogo 13.3 cha masharti ya jumla ya mkataba.

"Pia, nilibaini kwamba mkataba huu ulivunjwa mnamo Novemba 2019 na kazi za ujenzi kuhamishiwa kwenda Suma JKT. Hii inamaanisha kuwa fedha iliyotumika kugharamia kazi za ziada haitaweza kurudishwa na kuathiri mzunguko wa fedha kwenye miradi mingine," anabainisha.

CAG pia anasema mapitio ya usanifu, uboreshaji na ujenzi wa jengo la makao makuu ya Wakala wa Barabara (Tanroads) kwenye Kiwanja Na. 8 Kitalu 'F' katika eneo la Uwekezaji la Njedengwa, Manispaa ya Dodoma, yalibaini kuwa na dosari.

Anasema katika kipindi cha ukaguzi Januari mwaka huu, alibaini maendeleo ya ujenzi hayakuwa ya kuridhisha, yakiwa yamefikia asilimia 30 wakati asilimia 100 ya muda wa mkataba ukiwa umepita.

"Pia, nilibaini mkandarasi (TBA) alifanya kazi za ujenzi bila kuwapo kwa mkataba halali kutokana na wa awali kwisha muda wake tangu tarehe 19 Desemba 2019," anasema.

CAG pia anasema alibaini dosari katika usanifu na ujenzi wa makao makuu na Ofisi ya Kanda ya Tume ya Maadili katika Mkoa wa Dodoma.

Anasema kuwa katika ukaguzi wa mradi huo, alibaini kuwa ujenzi ulianza Januari 5, 2018 kabla ya mkataba kutiwa sainiwa Juni 14, 2019 (mwaka mmoja na nusu baadaye).

"Kwenye taarifa yangu ya mwaka uliopita (2017/18), nimeonyesha usimamizi duni wa fedha na vifaa vya ujenzi; uhaba wa wataalamu na mashine za ujenzi pamoja na utoaji mdogo wa fedha za mradi kutoka kwa washitiri (washirika), umechangia kwa kiwango kikubwa utekelezaji usioridhisha wa miradi ya ujenzi.

"Kupitia taarifa hiyo nilipendekeza Menejimenti ya TBA kubuni udhibiti wa ndani madhubuti kwenye usimamizi wa miradi, lakini hakuna maboresho yaliyoonekana katika kipindi hiki cha ukaguzi (2018/19).

"Pia nilibaini kuwa hadhi ya wakala imeendelea kuporomoka ambapo wakala umeondolewa kwenye miradi miwili mikubwa kutokana na utekelezaji duni. Miradi hiyo ni wa ujenzi wa nyumba za makazi ya Gereza la Ukonga na usanifu na ujenzi wa jengo la Ofisi ya NEC.

"Hii inadhoofisha ukuaji wa wakala kufikia uwezo wa kujitegemea kifedha. Hivyo basi, napendekeza Menejimenti ya TBA kuelekeza rasilimali zake katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma ya ushauri huku wakitengeneza mbinu sahihi zitakazowawezesha kufanya kazi za ujenzi kwa ufasihi," CAG anashauri.



Waumini wa kanisa kuu la Roho Mtakatifu Angalikana Dayosisi ya kati, wakishiriki meza ya sakramenti huku wakiwa kwenye foleni ya watu wachache ikiwa ni sehemu ya kujilinda na ugonjwa wa corona. **PICHA; PETER MKWAVILA**.


**AFRICAN MINERALS AND GEOSCIENCES CENTRE (AMGC)**

**JOB OPPORTUNITY**

**Chemist/Geochemist for instrumental Analytical Chemistry**

**Company Profile**

The African Minerals and Geosciences Centre (AMGC) formerly known as the Southern and Eastern African Mineral Centre (SEAMIC) was assigned by the International Conference on the Great Lakes Region (ICGLR) to host a laboratory for instrumental analytical chemistry. This laboratory will provide analytical data needed for the Analytical Fingerprint (AFP) to verify the origin of conflict minerals (cassiterite, Coltan, and wolframite). The German Federal Institute for Geosciences and Natural Resources (BGR) assigned by the German Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ) is supporting AMGC to set up this laboratory.

In this context, AMGC is seeking a qualified senior chemist/geochemist for setting up and running the AFP laboratory which will be equipped with a laser-ablation inductively coupled plasma-mass spectrometer (LA- ICP-MS) and a scanning electron microscope (SEM).

**Tasks and Responsibilities**

The senior chemist/geochemist will run the above mentioned analytical equipment and service it to the extent possible for a well-trained user. Training and steering for the position will be provided by BGR in the framework of ICGLR/BGR technical cooperation.

**The chemist/geochemist has the following tasks:**

- Receive, record and analyse samples from clients;
- Record, interpret and report results to the client;
- Knowledge of geochemistry and analysis of geological materials;
- Knowledge of environmental analysis;
- Be responsible for running the above mentioned analytical equipment to produce analytical data necessary for the AFP;
- Check the analytical quality of the obtained results;
- Perform adaption of the used methods if necessary;
- Support the development of additional applications of the equipment within the framework of the AMGC service portfolio;
- Perform the basic technical service for the above mentioned equipment;
- Organise technical support by the equipment manufacturer if necessary.

**Required qualification**

The successful applicant should demonstrate the following:

- Educated to BSc level at an internationally recognised unity in Chemistry or/and Geochemistry; MSc level will be an added advantage;
- More than 5 years of relevant work experience (including the application and development of modern instrumental analytical methods);
- Experience in mineralogy, inorganic instrumental analytical chemistry of chemometrics would be an advantage;
- Knowledge of environmental analysis;
- Working on AAS, ICP and XRF equipment will give an added advantage.
- Applicant must be a Tanzanian Citizen.

**Required skills**

The successful applicant should demonstrate the following:

- Fluency (written and oral) in English;
- Expert knowledge of standard office software (Excel, Word, PowerPoint) will be expected;
- Positive attitude towards learning and being trained by a BGR expert;
- High level of personal accountability and sense of responsibility.

**Submission of application**

Applications should include the following documents:

Application letter in English highlighting the candidate's motivation and describing how the candidate meets the essential qualifications and skills for the position;A detailed CV with contact information for the three referees (including their affiliation, position, e-mail and telephone numbers; support letters may also be attached); Certified copies of the MSc degree and other academic degrees, as well as other relevant certificates (e.g. training) and send to the Director General, African Minerals and Geosciences Centre (AMGC), P.O. Box 9573, Kunduchi Beach Area, Dar es Salaam, Tanzania; or yusuphhassani@seamic.org and timo.gawronski@bgr.de

**Deadline: 2 weeks from the day of advertisement.**


## ... abaini tatizo ununuzi mahema ya bil 6.3/- NEC

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika mkataba wa ununuzi wa mahema kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura wenye thamani ya Sh. bilioni 6.3 ulioingiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, iliyowasilishwa bungeni jijini hapa wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, anasema NEC haikufuata Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 katika kuingia mkataba huo.

Anabainisha kuwa Aprili 11, 2019, NEC iliingia mkataba Namba IE/018/2018-19/HQ/G/18 na mzabuni aitwaye Yell Ltd kwa ajili ya ununuzi wa mahema 2,237 yenye thamani ya Sh. 6,306,146,740.

Anasema mkataba ulitakiwa kutekelezwa ndani ya siku 60 kwa ajili ya maboresho ya daftari la kudumu la wapigakura, lakini alibaini utekelezaji wake ulikuwa na dosari tano ikiwa ni pamoja na kutofanyika kwa tathmini ya kina (Due diligence/post qualification) ya kumpata mzabuni.

"Ukaguzi ulibaini kuwa NEC haikufanya tathimini ya kina ili kubaini uwezo wa kifedha wa Mzabuni, utaalamu pamoja na vifaa kinyume cha kifungu cha 53 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016).

CAG pia anasema alibaini vipimo, maelezo na ubora (specifications and quality) wa mahema havikujumuishwa kwenye mchakato wa zabuni, akifafanua kuwa NEC ilishindwa kuvijumuisha katika nyaraka za zabuni (tender documents), hatua iliyosababisha mzabuni kuwasilisha mahema yasiyokuwa na ubora.

Katika ripoti hiyo, CAG pia anasema alibaini maoni ya Mwanasheri Mkuu wa Serikali hayakujumuishwa katika mkataba kinyume cha Kanuni ya 59(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

Vilevile, CAG anasema alibaini NEC ilichelewesha malipo ya awali kwa mzabuni, akifafanua kuwa tume ilichelewa kwa siku 60 kufanya malipo ya awali ya Sh. milioni 931 kwa mzabuni, hali iliyosababisha mzabuni kuchelewa kukabidhi mahema kwa siku 60.

"Pia, nilibaini mzabuni alishindwa kutekeleza mkataba kwani alipeleka mahema 880 kati ya 2,237 ya mkataba, sawa na asilimia 39.

"Licha ya kucheleweshwa kwa malipo ya awali kwa siku 60, mzabuni aliomba muda wa nyongeza ya muda wa mkataba, lakini Kamati ya Zabuni ya NEC katika kikao chake cha tarehe 6/11/2019, ilikataa kutoa nyongeza, kinyume cha kifungu cha 19 cha mkataba.

"Kutokana na upungufu uliobainika hapo juu, nilibaini kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa mahema. Hivyo, napendekeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhakikisha inasimamia kikamilifu mkataba huo, ili serikali ipate thamani halisi ya fedha," anashauri.

# Wanafamilia 4 wazama mtoni, wafa

**Na Neema Hussein,**
KATAVI

WATU wanne wa familia moja wamefariki dunia, baada ya chombo walichokuwa wakisafiria kuzama kwenye maji katika Mto Ugala wilaya ya Nsimbo mkoani Katavi.

Tukio hilo limetokea April 11, 2020 na miili yao ilipatikana Aprili 12, mwaka huu, katika kambi ya uvuvi Kalele iliyopo katika kijiji cha Katambike Kata ya Ugala.

Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema miili ya watu watatu imeshapatikana na mmoja anatafutwa.

Aliwataja waliokufa ni watoto Laurent Florence (15), ambaye alikuwa mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Katambike, Damiano Raphael (10), Daud Mabula (68) na Nicolaus Damiano (40), ambaye mwili wake haukupatikana.

Aidha, Kamanda huyo alisema watu hao ni wanandugu, na haijabainishwa vyema undugu wao.

"Watu hawa walivuka kwa mtumbwi katika mto huo na kuelekea upande wa pili mkoani Tabora kuweka mizinga ya nyuki katika msitu, lakini wakati wakirudi chombo hicho kilizidiwa maji na kuzama," alisema.

Tukio kama hilo liliwahi kutokea miaka 16 iliyopita, ambapo watu wanne pia walipoteza maisha katika eneo hilo, baada ya mtumbwi waliokuwa wakisafiria kuzama.




Waumini wa Kanisa la Enlightened Christian Gathering Church (ECG) kwa kupitia foundation ya baba yao wa kiroho Nabii Mkuu Shepherd Bushiri, wametoa msaada wa vitu vyenye thamani ya Sh. 1,600,000 ikiwa ni sehemu ya kusherehekea sikukuu ya Pasaka na watoto wenye mahitaji maalum. Mama Mtume Ivon Mtalemwa (kulia) na Mchungaji Kiongozi wa Dar es Salaam, Patrick Manda (wa pili kulia) wakikabidhi vitu hivyo kwa Mwakilishi wa Taasisi ya Young Councelling (YOKO) Joseph Ruzegama (kushoto) na mtoto Leah Rweyemamu (katikati). Shughuli hii ilifanyika Mbezi jijini Dar es Salaam juzi. Waumini hao pia walitembelea kituo kingine kilichopo Sinza kiitwacho Chakuama na kuwabariki watoto kwa misaada yenye thamani ya Sh. 1,300,000.. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sababu mbili kupungua deni matibabu ya India

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ametaja sababu mbili za kupungua kwa deni la serikali katika hospitali za rufani za India.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, anazitaja sababu hizo kuwa ni pamoja na Hospitali za Apollo kukataa kupokea wagonjwa wanaotibiwa kwa mkopo.

CAG anabainisha kuwa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeripoti matumizi yasiyolipwa ya Sh. bilioni 272,629,610,089 (bilioni 272.629) ambayo ni pamoja na ankara za matibabu za Sh. 19,174,817,593 (bilioni 19.175) kutoka hospitali za rufani za India.

"Ikilinganishwa na mwaka 2017/18, deni la matibabu la kiasi cha Sh. 29,172,371,931 (bilioni 29.172) limepungua kwa Sh. 9,997,554,338 (bilioni 9.997) ambazo zililipwa katika mwaka wa ukaguzi.

"Sababu za kupungua kwa deni hilo ni kuimarika kwa huduma za matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). Vilevile Hospitali za Apollo zilikataa kuchukua wagonjwa wanaohudumiwa kwa mkopo.

"Pia, idadi ya wagonjwa imeshuka kutoka wagonjwa 139 mwaka 2017/18 hadi kufikia wagonjwa 82 mwaka 2018/19, sawa na asilimia 41," alisema.

Tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano Novemba 5, 2015, huduma za matibabu ya kibingwa zimekuwa zikiimarishwa nchini, ili pamoja na mambo mengine, kupunguza idadi ya Watanzania wanaolazimika kupelekwa nje ya nchi kupata matibabu hayo.

Mpaka sasa, Tanzania inatoa huduma mbalimbali za matibabu ya kibingwa ikiwa ni pamoja na upandikizaji wa figo ambazo awali wagonjwa walilazimika kupelekwa ughaibuni, hasa hospitali za rufani za Apollo, India kupata matibabu hayo.

# CAG: Polisi hawajakusanya bil. 4.6/- makosa barabarani

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

JESHI la Polisi halijakusanya Sh. bilioni 4.6 zilizotokana na makosa ya barabarani katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19, imebainika.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, anasema amebaini kutokusanywa kwa kiasi hicho cha fedha.

Anasema amepitia taarifa ya makusanyo ya Jeshi la Polisi inayoishia Desemba 2019 na kubaini kiasi cha Sh. 4,570,783,000 kilichotakiwa kukusanywa kutokana na makosa ya barabarani kwa kipindi cha (2015/16 hadi 2018/19) hakikukusanywa, jambo ambalo ni kinyume cha Kanuni ya 57(2) ya Usimamizi wa Fedha ya Mwaka 2001 (iliyoboreshwa mwaka 2004).

Kanuni hiyo inawataka maofisa masuuli wote kuhakikisha wadaiwa wanakumbushwa kulipa madeni yao na wachukue hatua mbalimbali, zikiwamo za kisheria, ili makusanyo husika yanakusanywa.

"Kutokukusanywa kwa tozo za makosa ya barabarani kwa kipindi kirefu, kumechangiwa na kutokuwapo kwa mifumo thabiti inayoruhusu wavunjaji wa sheria za barabarani kuhuisha leseni zao bila kulipa malimbikizo ya madeni yanayotokana na uvunjaji wa sheria.

"Ni maoni yangu kwamba, kutokukusanya mapato kunainyima serikali kutumia fedha hizo katika shughuli nyingine. Nazishauri taasisi zinazohusika, kuhakikisha kwamba mpango mkakati unawekwa ili makusanyo yote yanayotokana na tozo za uvunjaji wa sheria barabarani yanakusanywa," CAG anapendekeza.

# TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA - NMB BANK PLC

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

NMB
Karibu yako

TZS Trilioni 4.9 Amana

TZS Trilioni 3.6 Mikopo

TZS Trilioni 6.4 Jumla ya Mali

Mapato yasiyo ya Riba 4% YoY

$£€¥ Mapato kutoka Fedha za kigeni 17% YoY

Faida baada ya kodi TZS Bilioni 145

27% YoY Tengo Mikopo Chechefu

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

## TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI Mwaka wa sasa 31.12.19 | KUNDI Mwaka uliopita 31.12.18 | BENKI Mwaka wa sasa 31.12.19 | BENKI Mwaka uliopita 31.12.18 |
|---|---|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 498,231 | 402,709 | 498,231 | 402,709 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 842,909 | 667,713 | 842,909 | 667,713 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 761,554 | 740,185 | 761,554 | 740,185 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 264,326 | 174,391 | 264,326 | 174,391 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 4,152 | 1,613 | 4,152 | 1,613 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 3,590,006 | 3,241,401 | 3,595,688 | 3,251,794 |
| 12 | Mali Nyingine | 214,160 | 179,581 | 383,191 | 212,052 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 239,169 | 265,700 | 203,044 | 227,607 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **6,417,427** | **5,676,213** | **6,556,015** | **5,680,984** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 33,446 | 20,770 | 33,446 | 20,770 |
| 18 | Amana za Wateja | 4,882,123 | 4,274,732 | 4,887,850 | 4,287,119 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 19,833 | 22,535 | 19,833 | 22,535 |
| 20 | Amana Maalumu | 14,595 | 17,953 | 14,595 | 17,953 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 33,355 | 35,019 | 33,355 | 35,019 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | - | - | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 117,530 | 75,649 | 247,104 | 62,174 |
| 28 | Madeni | 347,443 | 372,360 | 347,443 | 372,360 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **5,448,325** | **4,819,018** | **5,583,626** | **4,817,930** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **969,102** | **857,195** | **972,389** | **863,054** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 799,733 | 698,167 | 809,173 | 710,785 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 144,739 | 100,961 | 142,167 | 97,663 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,049 | 34,606 | 1,049 | 34,606 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,581 | 3,461 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **969,102** | **857,195** | **972,389** | **863,054** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 652,654 | 542,366 | 652,654 | 542,366 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 178,533 | 199,874 | 178,533 | 199,874 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 173,110 | 131,599 | 173,110 | 131,599 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 196 | 1,568 | 196 | 1,568 |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.1% | 15.1% | 14.8% | 15.2% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.8% | 5.9% | 4.8% | 5.9% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76.5% | 78.2% | 76.6% | 78.2% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.9% | 57.1% | 54.8% | 57.2% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 72.0% | 73.3% | 70.5% | 73.4% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 13.9% | 1.0% | 13.7% | 1.3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 13.1% | 3.2% | 15.4% | 3.2% |

## TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI Mwaka wa sasa 31.12.19 | KUNDI Mwaka uliopita 31.12.18 | BENKI Mwaka wa sasa 31.12.19 | BENKI Mwaka uliopita 31.12.18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 653,195 | 600,555 | 653,974 | 601,638 |
| 2 | Gharama za Riba | (130,820) | (109,615) | (136,333) | (109,615) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **522,375** | **490,940** | **517,641** | **492,023** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (100,410) | (137,305) | (100,410) | (137,305) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **204,409** | **195,823** | **204,409** | **195,876** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 25,554 | 21,894 | 25,554 | 21,947 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 169,153 | 166,282 | 169,153 | 166,282 |
| | 6.3 Gawio | - | 32 | - | 32 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 9,702 | 7,615 | 9,702 | 7,615 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(410,513)** | **(405,096)** | **(410,552)** | **(408,953)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (182,579) | (166,149) | (182,579) | (166,149) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (10,793) | (18,340) | (10,793) | (18,340) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (217,141) | (220,607) | (217,180) | (224,464) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **215,861** | **144,362** | **211,088** | **141,641** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (71,122) | (43,401) | (68,921) | (43,978) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **144,739** | **100,961** | **142,167** | **97,663** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa Faida/ (Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa | 168 | 182 | 168 | 182 |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **144,907** | **101,143** | **142,335** | **97,845** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,450 | 3,450 | 3,450 | 3,450 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 289 | 201 | 284 | 195 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 224 | 223 | 224 | 223 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.3% | 1.8% | 2.2% | 1.7% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 14.9% | 11.8% | 14.6% | 11.3% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.5% | 59.0% | 56.9% | 59.4% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.3% | 11.8% | 11.2% | 11.8% |

## TAARIFA YA UKAGUZI YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.19 | KUNDI Limbikizo la Mwaka Linganishi Mwaka Uliopita 31.12.18 | BENKI Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.19 | BENKI Limbikizo la Mwaka Linganishi Mwaka Uliopita 31.12.18 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 215,861 | 144,362 | 211,088 | 141,641 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 73,367 | 55,904 | 73,609 | 53,933 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (348,605) | (484,410) | (343,894) | (479,487) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (131) | (143) | (131) | (143) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 614,007 | 64,677 | 607,347 | 76,973 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (2,717) | (2,630) | (2,717) | (2,630) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 36,843 | 49,403 | 54,422 | 38,344 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (21,716) | (28,572) | (36,876) | (30,040) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (60,418) | (68,480) | (56,357) | (68,480) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 10,063 | (12,301) | 10,063 | (12,301) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **516,554** | **(282,190)** | **516,554** | **(282,190)** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (12,649) | (25,530) | (12,649) | (25,530) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 292 | 365 | 292 | 365 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (659,892) | (608,848) | (659,892) | (608,848) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 641,480 | 791,522 | 641,480 | 791,522 |
| | Mengineyo (bainisha) | (10,967) | (11,930) | (10,967) | (11,930) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(41,736)** | **145,579** | **(41,736)** | **145,579** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | 68,190 | - | 68,190 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (33,000) | (32,000) | (33,000) | (32,000) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (71,102) | (66,120) | (71,102) | (66,120) |
| | Mengineyo (bainisha) | (60) | 6,861 | (60) | 6,861 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(104,162)** | **(23,069)** | **(104,162)** | **(23,069)** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **370,656** | **(159,680)** | **370,656** | **(159,680)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 842,714 | 1,002,394 | 842,714 | 1,002,394 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **1,213,370** | **842,714** | **1,213,370** | **842,714** |

## TAARIFA YA UKAGUZI YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **808,448** | **-** | **33,725** | **881** | **863,054** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 142,167 | - | - | - | 142,167 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 33,725 | - | (33,725) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 168 | 168 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **951,340** | **-** | **-** | **1,049** | **972,389** |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **749,661** | **-** | **26,849** | **699** | **797,209** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 97,663 | - | - | - | 97,663 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (32,000) | - | - | - | (32,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (6,876) | - | 6,876 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 182 | 182 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **808,448** | **-** | **33,725** | **881** | **863,054** |

## TAARIFA YA UKAGUZI YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **799,128** | **-** | **33,725** | **4,342** | **857,195** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 144,619 | - | - | 120 | 144,739 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 33,725 | - | (33,725) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 168 | 168 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **944,472** | **-** | **-** | **4,630** | **969,102** |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **737,494** | **-** | **26,849** | **3,709** | **788,052** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 100,510 | - | - | 451 | 100,961 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (32,000) | - | - | - | (32,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (6,876) | - | 6,876 | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 182 | 182 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **799,128** | **-** | **33,725** | **4,342** | **857,195** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna<br>**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji** | | 30 Machi 2020 |
| Benedicto Baragomwa<br>**Kaimu Mkuu wa Fedha** | | 30 Machi 2020 |
| Juma Kimori<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | 30 Machi 2020 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na PricewaterhouseCoopers, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Margaret Ikongo<br>**Mkurugenzi** | | 30 Machi 2020 |
| Leonard Mususa<br>**Mkurugenzi** | | 30 Machi 2020 |

www.nmbbank.co.tz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Tuchukue tahadhari ya corona kikamilifu*

**UGONJWA** wa COVID 19 unabadilisha taratibu za maisha na kuifanya dunia kutumia teknolojia zaidi badala ya kuendeleza mambo ya zamani.

Ufanyaji kazi ofisini umebadilika zama hizi, hufanyika nyumbani na mtandao wa kompyuta ndicho kitendea kazi.

Vikao vya kupanga mipango au mikutano ya kikazi imeondolewa kinachotumiwa ni mawasiliano ya kimtandao, zipo barua pepe, skype, whatsap, zoom, teleconference na mawasiliano ya simu.

Ni jambo jema kwa nia ya kuwalinda na kuwaepusha wafanyakazi na maambukizi ya COVID 19 licha ya kwamba kuna gharama kubwa katika kukabiliana na janga la corona.

Ni wazi kuwa katika kufanyia kazi nyumbani kila mfanyakazi atahitaji kuwa na kompyuta mpakato badala ya zile za mezani.

Kampuni pia zitahitaji kugharamia bando kwa ajili ya mawasiliano na pia kuwalipia wi-fi (waifai) ili kufanikisha kazi zao na kuhakikisha kuwa uzalishaji unaendelea.

Ulinzi wa wafanyakazi sehemu za viwandani na ofisini ni jambo jema lakini pia hata mitaani kuuepusha umma na corona ni kitu kisichokwepeka hasa kwa kuhakikisha kuwa kunakuwa na huduma ya maji na sabuni za kunawa.

Tunayasema haya kwa sababu katika vituo vya mabasi kuna maji kwenye ndoo na sabuni ndani ya chupa zilizokuwa zimewekea maji.

Sabuni hizo ni za unga zilizochanganywa na maji na kwa hakika hakuna anayefahamu kipimo cha kutosha cha kuua wadudu wanaoweza kusababisha maradhi.

Tunachelea kusema kuwa kwa mifumo ya kunawia iliyoko mathalani kwenye vituo vya mabasi ni kama mzaha.

Unawaji mikono ule hauridhishi. Maji ni kidogo pengine hata robo ndoo, utokaji wake ni kidogo, lakini pia hata ndoo ya chini maji yanapomwagikia ni wa mashaka.

Tunasema ni wa mashaka kwa vile ndoo zinazopokea maji kutoka kwa wanaonawa ni ndogo na mara nyingi zimejaa na maji machafu huwamwagia wanaonawa, ambao huhisi kuwa wanachafuka badala ya kujitakasa na kujiepusha na corona.

Tunaamini kuwa serikali na hasa halmashauri za majiji, miji na miji midogo pamoja na wilaya zimeliona hilo na tunachoz-ishauri ni kununua mapipa angalau yenye lita 50 mpaka 100 au ndoo kubwa zenye ujazo wa lita zaidi ya 20 ili kuhifadhi maji yanayotiririka na pia kujenga mazingira bora ya sehemu za kusafirisha maji taka badala ya kuyaacha kuwachafua watu.

Tunaamini kuwa huu siyo wakati wa kutumia sabuni za unga zilizochanganywa na maji. Tunakumbusha kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Wakati umefika wa kuwapatia wananchi hasa vituoni sabuni zinazotakasa kama detol au dawa kama chlorine ili watu wanawe na kujihakikishia usafi bila hofu.

Tunaamini kuwa ni vyema pia utaratibu wa kusafisha magari ya abiria hasa yale yanayotumiwa kwenye usafiri wa umma.

Daladala au mwendokasi si salama na si suala la kuacha bila kuchukua hatua. Kuna haja pia ya kupulizia dawa magari haya na kuyatakasa kwani idadi ya wateja ni wengi na huenda baadhi wana maambukizi ambayo wanaweza kuyaacha kwenye viti, mlangoni au mabomba na sehemu nyingine wasafiri wanazozishika mara kwa mara.

Kwa vile serikali ina mamlaka inayosimamia vifaa tiba na dawa MSD, ichukue jukumu la kuwapatia wananchi sabuni zinazotakasa kuliko kuacha wananchi kunawia maji yenye sabuni kidogo ya unga ambayo huenda isiue hata vimelea vya magonjwa achilia mbali virusi vya corona.

Tunaomba pia serikali imulike nyumba za ibada , haina maana kuruhusu waumini wasali lakini bila tahadhari kwani wengi hunawa na maji kidogo tena bila sabuni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## *Wanafunzi mmesikia fursa ya vitabu hivi?*

Na Sabato Kasika

**WIZARA** ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, imetoa bure na kuweka mitandaoni vitabu vya shule za msingi na sekondari , ili wanafunzi wajisomee wakati huu wa likizo inayotokana na tishio la virusi vya corona.

Uamuzi huo wa serikali unatokana na kutambua kuwa wanafunzi wapo nyumbani na wanahitaji kuendelea kupata elimu hata wakiwa huko, hivyo inatumia huduma ya maktaba inayotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania.

Kwa mujibu wa Waziri Ndalichako, serikali imetoa huduma ya upatikanaji wa vitabu vyote kuanzia shule za msingi na sekondari katika maktaba bila malipo kwa njia ya mtandao.

Msisitizo ni kwamba wanafunzi wanatakiwa kutumia muda wao kusoma vitabu ambavyo serikali imewapa fursa bila gharama yeyote badala ya kuzurura mitaani na kujiweka katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa huo.

Nikirejea kwenye hoja, ni kwamba hata wazazi nao wanapaswa kujua ni kwa nini watoto wao wako likizo kwa sasa na kuwazuia kuzurura au kutembea ovyo, badala yake watulie nyumbani wajisomee.

Wazazi wapange muda kwa ajili ya kusimamia watoto wadogo wakati wa kusoma na kupumzika, kwani likizo hii siyo ya kuzurura au kwenda kusalimia ndugu na marafiki, bali ni ya kutulia nyumbani ili kupisha janga hilo.

Ikumbukwe kuwa virusi vya corona vinavyoendelea kuleta maafa sehemu mbalimbali dunia, na serikali iliamua kufunga shule ili kuwalinda watoto, hivyo wazazi nao wafanye sehemu yao ya kuhakikisha wanatulia nyumbani.

Wakichukulia tatizo hili kama jambo la kawaida na kuruhusu watoto kwenda kusalimia ndugu na marafiki badala ya kutulia wakisoma, wanaweza kusababisha ugonjwa huo kuingia nyumbani.

Kama kuna wazazi hawazingatii hilo wakati huu wa likizo ya dharura, huo ni uzembe wa hali ya juu, wajifunze kufuata maelekezo ya serikali, kwani lengo ni kuepusha watoto wasiambukizwe virusi vya corona.

Jukumu la mzazi au mlezi ni kuhakikisha mtoto wake anatulia nyumbani, wakati huu hadi hapo serikali itakapotangaza vinginevyo, kwani kuchukua hatua kama hizo kunaweza kusaidia janga hilo lisienee zaidi.

Mzazi na mlezi ndiyo wasimamizi wakuu wa kuhakikisha watoto wao wanazingatia hayo, lakini wakizembea na kuona ugonjwa wa corona kana hadithi tu, lengo la likizo litakuwa halijatimia.

Kuanzia mzazi, mlezi na mtoto, wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali na kupuuza taarifa za uzushi zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii zenye mzaha na upotoshaji.

Namna ya kupata taarifa sahihi ipo, hivyo hakuna haja ya kufuata za vijiweni, ambazo zinaweza kuwafanya wasizingatie maelekezo sahihi yenye lengo la kuepusha maradhi na pia kuwafanya wanafunzi watumie likizo vizuri.

Vilevile wanafunzi nao waambiwe ukweli ili watambue kuwa likizo hii ni maalum kwa ajili ya kupisha corona na siyo vinginevyo,ili wasisumbue kwa kutaka kwenda kutembea na kufurahi na wenzao.

Hajajulikana ni lini ugonjwa wa corona utaisha au utapata tiba au chanjo yake, hivyo wanafunzi wasipoteze muda, badala yake wautumie kwa kujisomea kwa bidii ili mwisho wa siku likizo hiyo ya dharura iwe na manufaa.

Ufungaji wa shule na vyuo, lengo lake ni kutaka wanafunzi watulie nyumbani wakiendelea kujisomea na siyo mwanya wa kutembea huku na kule, hali ambayo inaweza kusababisha wakajikuta wakiwa katika matatizo.

Serikali imetoa likizo na vitabu vya shule za msingi na sekondari katika mtandao bure, ili wanafunzi wajisomee wakati huu wakisubiri hali ya hewa itulie, hivyo ni muhimu likizo isipite bure.

Ni wazi mzazi au mlezi makini, hawezi kuruhusu mtoto wake kutoka nyumbani bila sababu za msingi, badala yake ataendelea kubaki ili kujisomea.

Tahadhari ni ya msingi kipindi hiki ambacho shule na vyuo vimefungwa, kuhakikisha watoto wanatulia nyumbani, hadi hapo serikali itakapotangaza kufunguliwa tena, hivyo kujisomea kupewe nafasi zaidi.

HABARI

Na Mwandishi Wetu,

DODOMA

# ‘Ushauri wa serikali haukuzingatiwa mkataba tata wa Uwanja wa Taifa’

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kutozingatiwa kwa ushauri wa serikali katika mkataba wa ukusanyaji wa mapato kwenye uwanja wa Taifa na Uhuru jijini Dar es Salaam ambao una matatizo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anasema kwamba, Juni 12, 2018, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu Na. 96) ilifanya makubaliano ya mkataba Na. ME/025/2017/2018/CR/04 na mzabuni Selcom Paytech PLC kwa ajili ya kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato katika viwanja vya Taifa na Uhuru kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Julai Mosi, 2018 hadi Juni 30, 2020 kwa gharama ya asilimia 4.45 ya mapato yanayotokana michezo na maonyesho.

Anabainisha kuwa wakati wa mchakato wa zabuni, wizara iliandika barua kwenda kwa taasisi mbalimbali za serikali (TanTrade, PCCB, TRA, Tazara, TRL and Tanesco) ili kujiridhisha na uwezo wa kampuni mbili (M/s Maxcom Africa Ltd and M/s Selecom Paytech PLC), zilizoshiriki kwenye mchakato wa zabuni.

“Hata hivyo, serikali kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CAB.105/260/01‘A’/20 ya Machi 23, 2018 iliagiza wizara kutokuingia makubaliano ya mkataba na kampuni tajwa hapo juu.

“Hata hivyo, wizara haikuzingatia ushauri wa serikali; na miezi mitatu baadaye, wizara iliingia mkataba na mzabuni Selcom Paytech PLC kinyume cha maagizo ya serikali.

“Pia, hakuna ushahidi wa kuwapo kwa mfanyakazi wa wizara mwenye taaluma ya Tehama anayesimamia stakabadhi zinazouzwa kupitia mfumo wa kielektroniki.

“Pia, wizara haina nyenzo ya kiTehama inayowezesha kujua idadi halisi ya watazamaji kwa kila tukio la michezo; zaidi ya kutegemea tu ripoti za muuzaji,” CAG anabainisha.

Anaongeza kuwa, kipengele cha nane cha mkataba kinamtaka mzabuni kuwasilisha mapato kwa walengwa ndani ya siku tatu. Hata hivyo, alibaini kuwa mapato ya Sh. 66,329,016 yalichelewa kuwasilishwa kwa kipindi kati ya mwezi mmoja na nusu hadi miezi sita, kinyume cha makubaliano ya mkataba.

“Wizara kushindwa kuwa na utaalamu wa kubaini mauzo yanayofanyika kwenye mfumo wa kielektroniki wa mzabuni wa kukusanya mapato, kunaweza kupeleka upotevu wa mapato kutobainika.

“Hivyo, naishauri wizara kuboresha ufuatiliaji wa mkataba wa makusanyo katika viwanja vya Taifa na Uhuru, ili serikali isipate hasara. Pia, nashauri ofisa masuuli azingatie miongozo ya serikali katika ununuzi,” CAG anapendekeza.



Mafundi wakitengeneza mtaro wa maji ya mvua pembeni mwa barabara inayoelekea kituo cha daladala cha Mawasiliano, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**



# Chadema yataka Dar ifungwe kwa wiki 3 maambukizi corona

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimependekeza Jiji la Dar es Salaam ambalo lina wagonjwa wengi wa virusi vya corona lifungwe kati ya siku 14 au 21 ili kupunguza idadi ya maambukizi.

Waziri Kivuli wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Cecilia Paresso, (Mbunge), alitoa mapendekezo hayo kupitia taarifa yake aliyoitoa jana.

Katika taarifa hiyo, Paresso alipendekeza jiji hilo lifungwe ili kutokuwa na mwingiliano na mikoa mingine pamoja na kuyafunga maeneo yote yenye mikusanyiko.

"Serikali ihakikishe vifaa vya kujikinga na virusi hivyo kama vile barakoa (mask) na vitakasa mikono (sanitizer) vinapatikana kwa bei nafuu kati ya Sh. 500 hadi 1000.

"Vifaa hivi vinaendelea kuuzwa ghali na kuadimika. Tunashauri serikali iondoe kodi kwa viwanda vya ndani vinavyotengeneza vifaa hivi ili uzalishaji uongezeke na kurahisisha upatikanaji wake."

Pia alisema serikali ihakikishe wataalamu wa afya wa hospitali za umma na binafsi wanapatiwa vifaa vyote muhimu vya kujikinga ili wasipate maambukizi.

"Maeneo yote yaliyotengwa kuwahudumia waathirika wa ugonjwa huu,serikali iwapatie posho maalum wataalamu hao wanapotekeleza majukumu yao katika mazingira magumu," alisema.

Kuhusu mikusanyiko, alisema wameendelea kuishuhudia katika maeneo mbalimbali kama vile minadani, makanisani, baa na kumbi za disco.

Pia, alisema wameshuhudia mikusanyiko inayofanywa na baadhi ya wakuu wa mikoa kinyume na maelekezo yanayotolewa na wataalam wa afya.

"Kuendelea kuiacha mikusanyiko kunaondoa kabisa dhana ya serikali kuamua kufunga shule na vyuo kama njia ya kukabiliana na janga hili," alisema.

Paresso alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinatakiwa kupewa vifaa vya kujilinda na kupendekeza Jeshi la Polisi lipunguze ukamataji holela ili kupunguza msongamano mahabusu.

"Serikali ione ulazima wa kuongeza idadi ya askari usalama barabarani ili kusimamia msongamano wa abiria katika vyombo vya usafiri hasa mabasi yaendayo mikoani na daladala kwenye miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha," alisema.

Kadhalika, amependekeza mipakani kuwe na karantini za kuwaweka wageni wanaoingia nchini kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya.

Paresso alipendekeza serikali iweke wazi bajeti halisi ya kupambana na corona ili Bunge lijadili kwa maslahi ya umma.

Vilevile, ameitaka serikali ieleze kiasi gani cha chakula imehifadhi kama dharura endapo utaendelea kwa muda mrefu na kuweka zuio la kukuuza nafaka nje kwa kipindi cha mlipuko.

Paresso ameishauri serikali kutoa ruzuku au kupunguza viwango vya riba za mikopo kwa kampuni kama ifanyavyo benki ili kuendelea kuzilinda biashara na ajira.




Mwendesha baiskeli akiwa amefunga mzigo wake kwa ustadi ili kuhakikisha haudondoki, alipokuwa akiusafirisha juzi eneo la Kimara Mwisho jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Corona yanusuru wacheza kamari kulala mahabusu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma, limewakamata watu 21 kwa kucheza kamari na kufanya mikusanyiko iliyozuiliwa na serikali kutokana na ugonjwa wa Corona katika sikukuu ya Pasaka.

Hata hivyo, watu hao wameachiwa kwa dhamana ikiwa ni jitihada za kuepuka msongamano kwenye vituo vya polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoani hapa, Gilles Muroto, alisema watu hao walikamatwa kwenye mitaa ya Ipagala na Swaswa ambapo walikuwa wakicheza kamari na kufanya mikusanyiko iliyozuiliwa.

"Tumewaachia kwa dhamana, na lengo la kuwaachia mahabusi hawa ni kutokana na kukwepa msongamano ambao serikali imekataza... kwenye Sherehe ya Pasaka vibaka wengi walijitokeza kufanyia uhalifu raia na, tumefanikiwa kuwadhibiti na kuwakamata,"alisema.

Aidha, alisema Jeshi hilo linaendelea na msako wa kuwasaka vibaka pamoja na wacheza kamari, mchezo ambao hauruhusiwi kisheria kutokana kuwaibia watu.

"Naomba vijana waache kucheza kamari kwa sababu ni mchezo ambao hauruhusiwi, yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria... kwa sasa mchezo huu ni sawa na kuwaibia watu wale wasiojua chochote kuhusu kamari, wao wanajua ni mchezo wa bahati nasibu," alisema.

Muroto alisema Polisi wanaendelea kuwasaka vibaka wanaovunja na kuiba vitu kwenye nyumba maeneo mbalimbali ya Jiji hilo, huku akiwataka wananchi kutoa taarifa ili kusaidia kudhibiti uhalifu.

"Hivi sasa askari wapo kila kona kusaka wahalifu hawa, kampeni hii ni endelevu tunataka kukomesha wizi na uzururaji unaofanywa na vijana," alisema.

# Maaskofu Seheba, Mkude wataka hadhari ya corona

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Morogoro, Godfrey Seheba na Mhashamu Askofu Telesphor Mkude wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, wamewataka waumini wa makanisa hayo kuchukua taadhari dhidi ya virusi vya homa ya corona.

Wametaka kupunguzwa idadi ya waumini makanisani na kunawa mikono kabla na baada ya kutoka makanisani.

Akizungumza katika ibada ya Pasaka iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Utatu Mtakatifu, Askofu Seheba alisema pamoja na kuwapo kwa mapinduzi ya sayansi na teknolojia, lakini bado ugonjwa huo umeshindikana kupatiwa tiba yake na kutaka waumini wa dini zote waendelee kuchukua taadhari.

"Tufuate maelekezo yanayotolewa na Serikali kwa ajili ya kujikinga na corona... na sisi kama kanisa tumeanza kuchukua tahadhari hiyo kwa kupunguza idadi ya waumini," alisema Askofu Seheba.

Naye Askofu Mkude ameishukuru Serikali kwa uamuzi wake kuruhusu madhehebu ya dini kuendelea kufanya ibada kwa kuzingatia tahadhari zote za kukabiliana na ugonjwa huo, lakini akataka kuongezeka kwa umakini kwa waumini hao.

Amesema Kanisa hilo limeweka na kuchukua tahadhari zote katika kipindi chote kuwa na utaratibu maalumu wa uendeshaji wa ibada ukiwamo ukaaji katika viti ndani ya kanisa na kuwekwa vitiririsha maji kwa ajili ya waumini kunawa mikono na sabuni.

Askofu Mkude alisema hayo wakati akitoa mahubiri katika ibada ya Pasaka kwenye Kanisa Kuu la Mtakatifu Patrice mjini Morogoro.

Alisema kutokana na maelekezo hayo na elimu inayotolewa na wataalamu wa afya na madaktari, waumini wa kanisa hilo wamekuwa wakiyatekeleza na mwitikio wake ni mkubwa .

Askofu Mkude, alisema ugonjwa huo umeanzia nchi zenye uwezo wa kiuchumi na kitatibu, hivyo viongozi wa dini nchini hawana budi kuzingatia maelekezo yote yaliyotolewa na Serikali ili kuhakikisha wananchi ambao ni wamumini wao wanakuwa salama.

Mkuu wa Morogoro, Loata Ole Sanare, aliwataka wakazi wa mkoa huo kuendelea na utaratibu wa kusherehekea sikukuu hiyo na nyinginezo wakiwa wametulia nyumbani.

Alisema, mkoa huo una barabara kuu zinazopitiwa magari yakiwamo mabasi kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Nyanda za Kusini, Kanda ya Kati na nchi jirani, hivyo suala la wananchi kuchukua tahadhari ni la muhimu.

Hata hivyo , alisema wakazi wa mkoa huo wamekuwa wakitii maagizo ya serikali ya kujiepusha na mkusanyiko na kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambuziki ya virusi vya corona.

Alisema wananchi wamekuwa wakizingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa afya kuhusu namna ya kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi hayo.

Hata hivyo, alisema bado wapo makondakta na madereva wasiozingatia agizo la Serikali, na kwamba wanaokaidi wanashughulikiwa na vyombo vya dola pamoja na kutozwa faini

## TANGAZO

# TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31/12/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka Ulio pita 31/12/2018 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 266 503 | 213 095 |
| 2. | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 1 105 509 | 962 928 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 2 372 006 | 2 947 788 |
| 12 | Mali nyingine | 172 095 | 213 637 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 165 546 | 165 672 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **4 081 659** | **4 503 120** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 1 317 863 | 1 092 657 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | | |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 8 750 | 318 121 |
| 28 | Madeni | 482 561 | 783 465 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1 809 174** | **2 194 243** |
| **30** | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **2 272 485** | **2 308 877** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji HISA uliolipiwa | 4 483 227 | 4 498 358 |
| 32 | Akiba ya mtaji | - | - |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (2 433 748) | (2 468 330) |
| 34 | Faida (hasara) ya kipindi husika | 65 654 | 105 046 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 157 352 | 173 803 |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| **37** | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2 272 485** | **2 308 877** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 174 259 | 90 145 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 65 412 | 57 058 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 56% | 51% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 7% | 3.1% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 180% | 270% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 58% | 65% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 58% | 65% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 17% | -292% |
| (vii) | Ongezeko la mali | -10% | 2% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31/12/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliopita 31/12/2018 |
|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya riba | 482 403 | 445 519 |
| 2. | Gharama za riba | (12 509) | (46 438) |
| 3. | Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2) | **469 894** | **399 081** |
| 4. | Madeni viza yaliyopitwa | | |
| 5. | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | (8 615) | (9 947) |
| **6.** | **Mapato yasiyo ya riba** | **199 081** | **321 078** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 199 081 | 321 078 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | - | - |
| **7.** | **Gharama zisizo na riba** | **(594 706)** | **(614 111)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (240 466) | (261 009) |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (354 240) | (353 102) |
| 8. | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **65 654** | **96 101** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | 19 696 | 28 830 |
| **10** | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **45 958** | **67 271** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | **-** | 37 775 |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **45 958** | **105 046** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 15 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 14.64 | 21 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.6% | 2.1% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.0% | 3% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 87% | 80% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 20% | 14% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31/12/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 65 654 | 96 101 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya mwanzo wa mwaka | (42 261) | 10 534 |
| | - Hasara Katika Mali | 31 368 | 48 017 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 575 782 | (1 034 555) |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - |
| | - Mabasiliko halisi katika amana | 225 205 | (3 187 914) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (338 200) | 107 625 |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 41 542 | 16 902 |
| | - Kodi iliyolipwa | | - |
| | - Mengineyo(bainisha) | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji** | **559 090** | **(3 943 290)** |
| **II:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | (30 616) | (111 242) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | | |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo | | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(30 616)** | **(111 242)** |
| **III:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | (15 130) | 3 388 222 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslilmu | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | (300 904) | (250 440) |
| | Mengnineyo(bainisha) | (16 451) | (72 364) |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(332 485)** | **3 065 418** |
| **IV:** | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslilmu | 195 989 | (989 114) |
| | Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/Mwaka | 1 176 022 | 2 165 136 |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/Mwaka** | **1 372 011** | **1 176 022** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 31/12/2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa | 4 498 358 | 0 | -2 363 284 | 2 836 | 27 536 | 143 431 | 2 308 877 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 45 958 | | | | 45 958 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | -15 131 | | | | 0 | | -15 131 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 27 536 | 0 | -27 536 | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | -48 394 | 48 394 | 0 | | 0 |
| Mengineyo | | | -29 910 | | 0 | -37 309 | -67 219 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4 483 227 | 0 | -2 368 094 | 51 230 | 0 | 106 122 | 2 272 485 |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | 1 110 136 | 0 | -2 498 748 | 112 | 18 415 | 0 | -1 370 085 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 105 046 | | | | 105 046 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 3 388 222 | | | | 0 | | 3 388 222 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | -2 724 | 2 724 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | -9 121 | | 9 121 | | 0 |
| Mengineyo | | | 42 263 | | 0 | 143 431 | 185 694 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4 498 358 | 0 | -2 363 284 | 2 836 | 27 536 | 143 431 | 2 308 877 |

Hesabu hizo hapo juu,ni kutoka kwenye hesabu za benki kwa mwaka ulioishia Disemba 31.2019, ambazo zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Makampuni kifungu 212 Sheria Na.12 ya 2002.
Hesabu hizi zimekaguliwa na TAC Associates na kupata hati safi

Hesabu hizi ziliapitishwa na bodi ya wakurugenzi na kusainiwa kwa niaba yake na:

| | |
|---|---|
| Mohamed Mwinguku | Mwenyekiti |
| Juma Namuna | Mkurugenzi |
| Mugwagi S. Steven | Meneja Mkuu |

# Waathirika mafuriko Kibiti waomba chakula

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

WAATHIRIKA wa mafuriko katika Kata ya Mtunda Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, wameomba kusaidiwa chakula pamoja na mbegu ambazo watazipanda kwenye mashamba yao maji yatakapoisha.

Akizungumza na Nipashe Diwani wa Kata ya Mtunda, Omari Twanga, alisema wananchi hao wana zaidi ya mwezi mmoja wakiwa kambini, hivyo huhitaji msaada zaidi.

**Wananchi hao wana zaidi ya mwezi mmoja wakiwa kambini, hivyo huhitaji msaada zaidi.**

Omari alisema kata hiyo ina vitongoji saba ambavyo vyote vimeathiriwa na maji, hivyo kuwafanya wananchi wake kuhama makazi yao, huku mashamba yakiwa yamejaa maji.

"Tangu mafuriko yametokea, wananchi hawa wako kwenye kambi, wengine wanaishi kwa ndugu, lakini wengi wao hawakuwa na sehemu ya kwenda... wanategemea msaada wa chakula kutoka Serikalini na wadau mbalimbali watakaojitokeza," alisema na kuongeza:

"Bado wanamahitaji ya chakula, wadau wenye uwezo wasaidie waathirika hawa kupata chakula na mbegu ambazo watazipanda kwenye mashamba yao maji yakiisha."

Mmoja wa wakazi wa Kibiti, Hamis Selemani, alisema, waathirika wa mafuriko wanatakiwa kuangaliwa namna ya kusaidiwa, kwani kwa sasa wako kwenye wakati mgumu kutokana na nyumba zao kujaa maji.

Hamis alisema waathirika hao kwa sasa wanahitaji chakula pamoja na mbegu kwani kuna hatari ya kukumbwa na baa la njaa kutokana na mazao yao kusombwa na maji.



Mwenyekiti wa Chama cha Walimu wilaya ya Ushetu mkoani Shinyanga, Juma Nyakanyeye, akizungumza na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa chama hicho wa kuwachagua viongozi wapya juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# RC Sanare aagiza Tawa, Tanapa kuwaondoa tembo kwenye makazi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, ameziagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa) na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) Mikumi wilayani Kilosa kushirikiana na maofisa wa wanyamapori wa wilaya na mkoa kuwaondoa tembo wanaozagaa katika makazi ya watu na kwenye shamba.

Lengo ni kuwawezesha wakazi wa maeneo hayo kuendelea na shughuli za uzalishaji mali.

Ole Sanare alitoa agizo hilo katika kikao maalumu alichokiitisha wilayani Mvomero kilichowakutanisha maofisa waandamizi wa Tawa na Tanapa- Mikumi, madiwani, wenyeviti na watendaji wa kata saba za wilaya hiyo, ambazo zinaathiriwa na kuvamiwa na tembo mara kwa mara.

Alisema tembo hao wamekuwa wakitoka ndani ya hifadhi na kwenda umbali wa kilometa kuanzia 10 hadi 20 kwenye maeneo ya makazi ya watu na kusababisha pia uharibifu wa mazao na kuhatarisha maisha ya watu, na miaka ya karibuni wamewahi pia kusababisha vifo vya watu.

Kufuatia hali hiyo, alizitaka taasisi hizo za Serikali zinazohusika na wanyamapori kuchukua hatua za kusimamia jambo hilo kwani wananchi wamekuwa washiriki kikamilifu kutoa taarifa za wanyamapori wanapoingia maeneo hayo bila ya wao kuchukua hatua za kuwadhuru.

" Hivi sasa wilaya zote za mkoa wa Morogoro kuna changamoto ya tembo, ni wakati sasa wa Tanapa na Tawa kuweka mpango endelevu ili kuwathibiti tembo kuingia kwenye makazi ya wananchi na kuharibu mashamba ya mazao," alisema Sanare.

Aliwataka wananchi wanapowaona wanyamapori wakiwamo tembo kuacha kuwaua, kwa kuwa kufanya hivyo watakuwa wanavunja sheria na wakibainika sheria itachukua mkondo dhidi yao kwani jukumu la kuwaondoa wanyama hao katika makazi yao shambani ni ya askari wa Tanapa na Tawa au maofisa wanyamapori.

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi wa Tanapa, Dominick Tarimo, alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo, kumeundwa kikosi maalumu chenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu wa mazao, wakiwamo tembo wanaovamia maeneo ya makazi ya watu.

Alisema , kikosi hicho maalumu kimepewa jukumu la kuwarejesha hifadhini wanyamapori wanaoonekana wamevuka kutoka hifadhini kwenda katika makazi ya watu, hivyo aliwaomba wananchi, viongozi wa vijiji vya kata kutoa ushirikiano wa karibu na kikosi hicho.

# Washauriwa kubadili muda wa ununuzi bidhaa sokoni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANUNUZI wa bidhaa za majumbani kwenye soko la Mawenzi lililopo Manispaa ya Morogoro, wameshauriwa kubadilisha ratiba ya kufanya ununuzi badala ya kufanya asubuhi pekee.

Hali hiyo imekuwa ikisababisha msongamano wa watu sokoni hapo hasa kwenye kipindi hiki cha ugonjwa wa Covic-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Mwenyekiti msaidizi wa soko hilo, Peter Ryoba, alisema jana kuwa, wanunuzi wengine wanaweza kwenda asubuhi na wengine wanaweza kwenda sokoni majira ya mchana na pengine jioni, na kupata mahitaji yao yote bila kukosa na hivyo kuwa katika hali salama kiafya muda wote.

Pia aliwashauri wanunuzi hao kuona haja ya kununua bidhaa kiasi cha kutosha siku tatu hadi wiki ili akiba hiyo iwasaidie kupata muda wa kutulia nyumbani hasa katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covic-19.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa soko hilo, Ramadhani Mohamed, aliuomba uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kuona haja ya kuwawekea majaba kwa ajili ya kuwekea maji ya kunawa wateja kutokana na ndoo zilizopo kuisha maji mapema na maji kupatikana kwa shida kutokana mgawo.

Alisema wateja wanaofika sokoni hapo ni zaidi ya 3,000 kwa siku ambao wamekuwa wakitii suala la kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni wanapoingia sokoni kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa na pale maji yanapokwisha huwaweka viongozi katika wakati mgumu.

"Jaba lina uwezo wa kuchukua ndoo za maji mbili na nusu hadi tatu, linaweza kusaidia kunawisha wateja kwa siku nzima na pengine kwa siku inayofuata na kuepuka usumbufu uliopo," alisema Mohamed.

Hata hivyo, wameishukuru Manispaa kuwawekea vitakasa mikono vya kutosha kwa kuwa awali walikuwa na shida kutokana na bei kubwa ya Sh. 3,500 kwa ndogo na kimoja kutumika kwa siku moja na kusababisha wafanyabiashara kushindwa kununua kwa wakati.

Nipashe
TESA
Jumanne Aprili 14, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 14.




Viuatilifu vilivyo kitisho uhai wa mkulima, mlaji

ELIMU

# Corona inavyoliamsha taifa kuboresha Tehama shuleni

**NA REUBENI LUMBAGALA.**

WANAFUNZI wa ngazi zote kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu, bado wapo kwenye mapumziko ya mwezi mmoja kudhibiti maambukizi ya ugonjwa homa ya mapafu nchini Covid-19.

Mapumziko haya yamekuja kufuatia kauli ya serikali iliyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliyeagiza wanafunzi wote wapumzike kwa muda wa mwezi mmoja ili kuepusha kuenea kwa ugonjwa wa corona kwani taasisi za elimu zinajumuisha mikusanyiko mikubwa ya watu ambayo ni hatari katika kusambaa kwa maradhi hayo.

Ndiyo maana sasa ni wakati wa kufikiria matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ambayo inaonekana kuwa ndiyo nyenzo muhimu katika kuchagiza ufundishaji na ujifunzaji hasa kwenye dunia hii ya sayansi na teknolojia.

Tehama inajumuisha matumizi ya kompyuta, kompyuta mpakato, redio na runinga katika kupata habari na mawasiliano mbalimbali ambayo ni muhimu kwa ujifunzaji bora.

Vifaa hivi vinachangia asilimia kubwa ufundishaji kwa kutumia Tehama hasa pale kompyuta zinapounganishwa na mtandao wa intaneti.

Kwa sehemu kubwa, taasisi za vyuo vya kati na vyuo vikuu vimepiga hatua katika matumizi ya Tehama kwa ujifunzaji na ufundishaji lakini changamoto kubwa ipo kwa upande wa shule za msingi na sekondari.

Hii inatokana na ukweli kuwa shule za msingi na sekondari ni nyingi na zipo vijijini na kwenye kata kote nchini, hivyo kufanya mahitaji ya huduma ya Tehama kufundishia kuwa kubwa mno.

Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo ya sekta ya elimu katika kusambaza kompyuta katika baadhi ya shule, kujenga vyumba vya kujifunzia kompyuta , somo la Tehama kufundishwa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati hadi vyuo vikuu, bado shule nyingi hazijafikiwa na huduma hiyo kwa maana ya vifaa na miundombinu wezeshi.

Ujifunzaji na ufundishaji unaweza kufanyika vizuri bila kuleta athari ya kuenea wa ugonjwa wa corona kupitia Tehama ambapo wanafunzi wanaweza kufuatilia hatua zote za ufundishaji unaofanywa na walimu kupitia kompyuta, redio, runinga na simu janja (smart phones).



Wanafunzi wanaposoma kwa mtandao hupunguza gharama nyingi ikiwamo karatasi kwa ajili ya kuandaa machapisho mbalimbali, hata uwezekano wa kuambukizwa magonjwa kurona na kujazana madarasani. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa sehemu kubwa, taasisi za vyuo vya kati na vyuo vikuu vimepiga hatua katika matumizi ya Tehama kwa ujifunzaji na ufundishaji lakini changamoto kubwa ipo kwa upande wa shule za msingi na sekondari.

Hii itapunguza athari za wanafunzi kukaa nyumbani bila kupata maarifa, stadi na ujuzi kutoka kwa walimu wao.

Kutokana na unyeti wa sekta ya elimu katika maendeleo ya nyanja zote, ni lazima iwekwe mikakati ambayo itanusuru sekta ya elimu hata kama kutatokea majanga kama hili la Corona lilivyoathiri ratiba na mihula ya elimu nchini. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali (Tamisemi), wanapaswa kuwa na mikakati ya kuhakikisha kila shule ya msingi na sekondari inakuwa na vifaa vya kufanikisha ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia Tehama.

Aidha, wizara hizi ziangalie uwezekano wa kuwashirikisha wadau wa elimu katika kufanikisha upatikanaji wa vifaa vya Tehama ili wanafunzi waweze kujifunza kidigitali, si katika kipindi hiki cha janga la corona pekee bali kwa kuzingatia kasi kubwa ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na namna Tehama inavyotumia katika kuhakikisha wanafunzi wanajifunza wakiwa ndani na hata nje ya mazingira ya shule.

Wizara ya Nishati pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) waendeleze kasi ya kusambaza nishati ya umeme kwa maeneo yote ya mijini na vijijini bila kusahau kuziunganishia shule za msingi na sekondari nishati ya umeme ambayo bila uwepo wa nishati hiyo, kazi ya ujifunzaji kwa kutumia Tehama itashindikana. Miongoni mwa vipaumbele vyao iwe ni pamoja na kuziunganishia taasisi za elimu nishati hiyo.

Mitandao ya simu ishiriki katika jambo hili kwa kuziunganishia baadhi ya shule huduma ya intaneti kwa gaharama ndogo au bure ili walimu na wanafunzi waweze kutumia vifaa hivyo kwa mawanda mapana kupitia uungwanishwaji wa huduma ya intaneti.

Halikadhalika, mitandao ya simu iendelee na utamaduni bora waliokuwa nao wa kugawa kompyuta mashuleni, kwani kompyuta ni nyenzo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya mtandao.

Kwa upande wa wazazi na walezi, wafuatilie vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kufahamu njia ambazo watoto wao wanaweza kujifunza wakiwa nyumbani kwa kutumia Tehama. Wapo baadhi ya wazazi na walezi nchini wanatumia Tehama katika kuwasaidia watoto wao kujifunza kwa mtandao wakiwa nyumbani katika kipindi hiki cha mapumziko mafupi. Kwa kufanya hivi, imewasaidia watoto wao kuendelea kujifunza wakiwa nyumbani na hivyo kutokupoteza muda bure.

Jambo la msingi ni kila mwananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona kwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya, huku kila Mtanzania kwa imani yake kumuomba Mungu ili ugonjwa uishe na shughuli nyingine za kimaendeleo ziweze kwenda kama ilivyokuwa awali. Mungu iponye Tanzania na dunia na maradhi haya ambayo hadi sasa Watanzania 46 wamepata tatizo hilo.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**
**Maoni: 0764 666349.**

TANGAZO

# CRDB BANK PLC

**TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA**

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni Za Mabenki Na Taasisi Za Fedha (UONESHAJI) ya mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE - 31 DESEMBA 2019
(Kiasi kwa Shilingi Milioni)

| | | GROUP | | BANK | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 |
| A. | MALI | | | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 333,796 | 311,424 | 329,341 | 308,895 |
| 2. | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 430,219 | 389,567 | 424,121 | 382,268 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,412,843 | 1,238,083 | 1,281,392 | 1,181,132 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 309,807 | 324,811 | 333,689 | 344,454 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 13,870 | 20,887 | 13,087 | 17,899 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | 46 | - | 46 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 4,520 | 3,516 | 4,520 | 3,516 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 3,382,024 | 3,126,733 | 3,325,613 | 3,061,544 |
| 12 | Mali Nyingine | 358,162 | 312,360 | 351,669 | 301,817 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 8,135 | 7,013 | 30,424 | 29,424 |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 343,872 | 300,947 | 331,432 | 288,355 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **6,597,248** | **6,035,387** | **6,425,288** | **5,919,350** |
| B. | DHIMA | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 33,011 | 3,994 | 14,315 | 3,994 |
| 18 | Amana za Wateja | 5,150,078 | 4,662,450 | 5,016,673 | 4,558,366 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 44,353 | 24,724 | 44,353 | 24,724 |
| 21 | Maagizo ya Malipo /Fedha za Kuhamisha | 6,590 | 2,674 | 6,521 | 2,068 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1,590 | 1,200 | 734 | 761 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 48,793 | 31,363 | 46,794 | 30,373 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 29,726 | 24,046 | 29,349 | 23,542 |
| 27 | Dhima Nyingine | 80,546 | 52,255 | 82,738 | 63,061 |
| 28 | Madeni | 329,492 | 459,061 | 329,492 | 459,061 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **5,724,179** | **5,261,767** | **5,570,969** | **5,165,950** |
| **30** | **MALI/ DHIMA HALISI (16 kutoa 29)** | **873,069** | **773,620** | **854,319** | **753,400** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 65,296 | 65,296 | 65,296 | 65,296 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yalibakizwa | 499,262 | 425,095 | 484,535 | 405,403 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 120,145 | 64,132 | 122,646 | 69,588 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 188,366 | 219,097 | 181,842 | 213,113 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **873,069** | **773,620** | **854,319** | **753,400** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,710,053 | 767,151 | 1,703,513 | 764,099 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 200,430 | 282,084 | 199,829 | 281,642 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 159,071 | 186,645 | 158,635 | 186,425 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwianao wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 13% | 13% | 13% | 13% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6% | 9% | 6% | 9% |
| (iii) | Uwianao wa Mikopo Ghafi Halisi na Jumla ya Amana | 68% | 71% | 69% | 71% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 51% | 52% | 52% | 52% |
| (v) | Uwianao wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77% | 78% | 77% | 78% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 11% | 8% | 11% | 8% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 9% | 2% | 9% | 2% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA - 31 DESEMBA 2019
(Kiasi kwa Shilingi Milioni)

| | | GROUP | | BANK | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwaka wa Sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 | Mwaka wa Sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 |
| 1. | Mapato ya Riba | 638,503 | 586,288 | 619,164 | 567,431 |
| 2. | Gharama za Riba | (116,308) | (143,444) | (111,563) | (135,804) |
| 3. | Mapato Halisi ya Riba ( 1 kutoa 2) | 522,195 | 442,844 | 507,601 | 431,627 |
| 4. | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (91,503) | (114,669) | (91,487) | (114,365) |
| **6.** | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **251,523** | **219,255** | **247,254** | **209,884** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 38,660 | 31,326 | 37,860 | 30,428 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 204,418 | 173,198 | 194,475 | 166,580 |
| | 6.3 Gawio | 30 | - | 6,530 | - |
| | 6.3 Mapato Mengine | 8,415 | 14,731 | 8,389 | 12,876 |
| **7.** | **Gharama Zisizo za Riba** | **(507,530)** | **(448,313)** | **(488,431)** | **(423,355)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (260,517) | (210,517) | (252,128) | (195,156) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (26,048) | (19,433) | (25,704) | (25,348) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (220,965) | (218,363) | (210,599) | (202,851) |
| 8. | Faida / (Hasara) Halisi ya Uendeshaji | 174,685 | 99,117 | 174,937 | 103,791 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (54,540) | (34,985) | (52,292) | (34,203) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **120,145** | **64,132** | **122,645** | **69,588** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | **328** | **9,922** | **(833)** | **9,672** |
| | | 328 | 9,922 | (833) | 9,672 |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **120,473** | **74,054** | **121,812** | **79,260** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 3,467 | 3,101 | 3,352 | 2,868 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 46.0 | 24.6 | 46.9 | 26.6 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 240 | 234 | 237 | 231 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i)Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.8% | 1.6% | 2.9% | 1.8% |
| | (ii)Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 14.7% | 8.2% | 15.4% | 9.1% |
| | (iii)Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 64.4% | 66.8% | 63.5% | 64.7% |
| | (iv)Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 10.9% | 10.1% | 10.8% | 10.0% |

Hapo juu ni taarifa za Fedha za Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2019, ambazo zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya makampuni,Namba 12 ya mwaka 2002 CAP 212.

Taarifa hizi za Fedha zimekaguliwa na wakaguzi wa nje Ernst&Young Certified Public Accountants (T) na kupata hati safi .

Taarifa hizi za Fedha zimepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi na kusainiwa kwa niaba yao na:

| | |
|---|---|
| Dr. Ally H. Laay | Mwenyekiti wa Bodi |
| Mr. Abdulmajid M. Nsekela | Mkurugenzi Mtendaji |
| Mr.Hosea E.Kashimba | Mjumbe wa Bodi |
| Tarehe: | 27 Machi 2020 |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA - 31 DESEMBA 2019
(Kiasi kwa Shilingi Milioni)

| | | GROUP | | BANK | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwaka wa Sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 | Mwaka wa Sasa 31/12/2019 | Mwaka Uliopita 31/12/2018 |
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 174,685 | 99,117 | 174,937 | 103,791 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | Hasara katika Mali | 166,488 | 167,823 | 163,138 | 165,890 |
| | Badiliko halisi katika Mikopo | 133,768 | 71,728 | 128,593 | 75,721 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (388) | 736 | (362) | 885 |
| | Mabadiliko Halisi katika Amana | 540,688 | 322,161 | 472,960 | 309,361 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (91,459) | (69,478) | (17,943) | (62,676) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 17,550 | 1,212 | 8,791 | (7,187) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (79,230) | (57,205) | (78,759) | (55,775) |
| | Kodi iliyolipwa | (49,024) | (43,703) | (48,871) | (42,937) |
| | Mengineyo (bainisha) | (551,137) | (491,585) | (538,026) | (478,442) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **261,941** | **806** | **264,458** | **8,631** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | | | |
| | Gawio Lilopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (36,395) | (92,542) | (35,731) | (91,708) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 1,184 | 233 | 1,037 | 126 |
| | Ununzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (881) | (13,459) | (759) | (13,269) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | (4,118) | (121) | (4,028) | (121) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Uwekezaji** | **(40,210)** | **(105,889)** | **(39,481)** | **(104,972)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (157,389) | (247,461) | (157,389) | (247,461) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lilolipwa kwa Fedha Taslimu | (20,895) | (13,012) | (20,895) | (13,012) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | 715 | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **(178,284)** | **(259,758)** | **(178,284)** | **(260,473)** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | Ongezeko / (Punguzo) Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 43,447 | (364,841) | 46,693 | (356,814) |
| | Fedha Taslimu na Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 703,651 | 1,068,492 | 690,723 | 1,047,537 |
| | **Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/Mwaka** | **747,098** | **703,651** | **737,416** | **690,723** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA - 31 DESEMBA 2019
(Kiasi kwa Shilingi Milioni)

GROUP

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa-31/12/2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | | | | | | | |
| -Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 489,226 | - | 31,020 | 29,764 | 773,620 |
| -Maabadiliko ya mwanzo wa mwaka | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **489,226** | **-** | **31,020** | **29,764** | **773,620** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 120,145 | - | - | - | 120,145 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 328 | 328 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (20,894) | - | - | - | (20,894) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 30,195 | - | (30,325) | - | (130) |
| Mengineyo | - | - | 735 | - | - | (735) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **619,407** | **-** | **695** | **29,357** | **873,069** |
| **Mwaka uliopita-31/12/2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | | | | | | | |
| -Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 463,424 | - | 27,217 | 19,209 | 733,460 |
| -Maabadiliko ya mwanzo wa mwaka IFRS 9 | - | - | (30,063) | - | - | - | (30,063) |
| - Kodi | - | - | 8,931 | - | - | - | 8,931 |
| - Nyinginezo | - | - | (107) | - | - | - | (107) |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **442,185** | **-** | **27,217** | **19,209** | **712,221** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 64,132 | - | - | - | 64,132 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Halisi | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | 9,922 | 9,922 |
| Gawio lililolipwa | - | - | (13,059) | - | - | - | (13,059) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (3,399) | - | 3,803 | - | 404 |
| Mengineyo | - | - | (633) | - | - | 633 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **489,226** | **-** | **31,020** | **29,764** | **773,620** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA - 31 DESEMBA 2019
(Kiasi kwa Shilingi Milioni)

BANK

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa-31/12/2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | | | | | | | |
| -Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 474,991 | - | 30,195 | 24,604 | 753,400 |
| -Maabadiliko ya mwanzo wa mwaka | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Halisi | 65,296 | 158,314 | 474,991 | - | 30,195 | 24,604 | 753,400 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 122,646 | - | - | - | 122,646 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | (833) | (833) |
| Gawio lililolipwa | - | - | (20,894) | - | - | - | (20,894) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 30,195 | - | (30,195) | - | - |
| Mengineyo | - | - | 243 | - | - | (243) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **607,181** | **-** | **-** | **23,528** | **854,319** |
| **Mwaka uliopita-31/12/2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| -Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 442,494 | - | 26,796 | 15,135 | 708,035 |
| -Maabadiliko ya mwanzo wa mwaka IFRS 9 | - | - | (29,772) | - | - | - | (29,772) |
| - Kodi | - | - | 8,931 | - | - | - | 8,931 |
| - Nyinginezo | - | - | 5 | - | - | - | 5 |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **421,658** | **-** | **26,796** | **15,135** | **687,199** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 69,588 | - | - | - | 69,588 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 9,672 | 9,672 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (13,059) | - | - | - | (13,059) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (3,399) | - | 3,399 | - | - |
| Mengineyo | - | - | 203 | - | - | (203) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **474,991** | **-** | **30,195** | **24,604** | **753,400** |

CRDB BANK PLC

TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni Za Mabenki Na Taasisi Za Fedha (UONESHAJI) ya mwaka 2014

## Muhtasari wa Taarifa za Fedha
(Kiasi kwa Shilingi Milioni)

| | 2018 | 2019 | Ongezeko |
|---|---|---|---|
| Mikopo | 3,126,733 | 3,382,024 | 8.2% |
| Mali | 6,035,387 | 6,597,248 | 9.3% |
| Amana za Wateja | 4,691,168 | 5,227,442 | 11.4% |
| Fedha za Wanahisa | 773,620 | 873,069 | 12.9% |
| Faida baada ya Kodi | 64,132 | 120,145 | 87.3% |
| Mapato Halisi ya Riba | 442,844 | 522,196 | 17.9% |
| Mapato yasiyo ya Riba | 219,255 | 251,524 | 14.7% |
| Idadi ya WAKALA | 5,080 | 12,828 | 152.5% |

**Tunathamini na kujali afya yako na wale uwapendao.**

Katika kuendelea kupambana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), nawa mikono yako kwa sabuni na maji safi, epuka mikusanyiko ya watu na fanya miamala kwa **SimBanking, TemboCard, Internet Banking** na **CRDB WAKALA** kwa usalama na haraka, muda wowote, mahali popote.

Piga *150*03# au Pakua SimBanking App kupitia App Store Google play

CRDB BANK

Tunakusikiliza

SAYANSI

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Viuatilifu vilivyo kitisho uhai wa mkulima, mlaji

MVUA zinazoendelea kunyesha zimeleta neema kwani wakulima wengi wana imani kuwa kilimo kitafanikiwa. Ukulima ni kazi inayowalisha watu wote iwe hapa Tanzania ama kwingineko duniani kwenye wakazi zaidi ya bilioni 7.8 ambao huishi wakitegemea mkulima awape chakula.

Kwa mujibu wa mtandao wa 'Population Matters' dunia ina watu bilioni 7.8 na hao wote ni lazima walishwe na mkulima, lakini kilimo kina madhara kwani watu takribini 200,000 wanaopoteza maisha kila mwaka kutokana na matumizi ya kemikali za kilimo za viuatilifu, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani kutokana na kutumia viuatilifu mbalimbali.

Wakulima hawa wanajizatiti kutumia viuatilifu, pembejeo kama mbolea, mbegu za kisasa na zinazovumilia ukame, zinazozaa sana na kukomaa mapema ili kuzalisha chakula cha kulisha watu mbalimbali wa dunia hii yenye idadi kubwa ya walaji kuliko walimaji.

Matumizi ya viuatilifu ni changamoto kubwa kwa wakulima, huenda wengi wanakufa kutokana na kutofahamu namna bora ya kutumia dawa hizo, kwa mfano wakulima wanapoteza maisha kutokana na athari zinazotokana na matumizi ya sumu za kuulia wadudu na kwamba kuna mambo mengi yanayoweza kuchangia kufa kwao.

Mathalani, matumizi ya teknolojia duni katika kilimo yanaweza kusababisha walimaji wengi kupoteza maisha wakati wakiwekea mimea viuatilifu, wapo watu wananyunyuzia mahindi dawa lakini hawafuniki midomo wala pua matokeo yake sumu huingia mwilini kupitia njia za hewa.

Hali hiyo ikiendelea kwa miaka mingi husababisha madhara, linasema Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), lakini pia wakulima hawatumii vifaa vya kujikinga kama glovu, mavazi wala hawazingatii muda wa kuweka dawa.

Baadhi hufanya kazi hiyo kwa muda mrefu bila kujali kuwa sumu hizo huwadhuru. Jambo jingine ni ukosefu wa elimu ya kuhifadhi dawa au kemikali hizo hatarishi ambazo licha ya kwamba ni sumu wakulima wengi hawako makini kwenye kutunza. Wapo wanaoziweka pengine chini ya miti, darini na hata kuzifukia chini ya ardhi bila kuzifunika na kuzihifadhi kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu. Dawa hizo hupata joto au utunzaji huo huzifanya kuwa sumu zaidi au kupungua nguvu.

Jambo jingine linalohatarisha maisha ya wakulima ni usafirishaji wa kemikali hizi, kutoka sehemu moja kwenye shambani. Huziweka kwenye chupa za maji na hawatumii njia sahihi wala vifaa vya kuhifadhi ili kusafirisha. Kadhalika ukosefu wa mavazi maalumu ya usalama wakiwa kazini na matumizi yasiyokuwa sahihi ya dawa hizi za kuua wadudu wanaoshambulia na kuangamiza mazao huwaangamiza watumiaji pia.




Wakulima wanaponunua viuatilifu na kemikali za shambani ni vyema kuuliza na kupata maelezo sahihi ya namna ya kuzitumia, kuzitunza na kuziharibu. **PICHA: MTANDAO**

> Mara nyingi katika maeneo ya shambani wakulima hutumia dawa za kuchanganya kwenye maji ili kudhibiti wadudu wanaoangamiza mazao mathalani mahindi.

Mara nyingi katika maeneo ya shambani wakulima hutumia dawa za kuchanganya kwenye maji ili kudhibiti wadudu wanaoangamiza mazao mathalani mahindi. Katika kuchanganya maji na kiuatilifu wakulima wengi huzidisha dawa matokeo yake mahindi huungua na kusababisha hasara. Katika mazingira hayo inadhihirisha jinsi ambavyo wakulima hawafahamu kipimo halisi na ni kwa namna gani pamoja na mimea hata wao hudhurika.

Wakati mwingine ni rahisi kuona kuwa athari za matumizi mabaya ya madawa ya kilimo imekuwa ikiongezeka kutokana na kukua kwa sekta ya viwanda vinavyozalisha sumu za kuua wadudu wa mimea pamoja na ongezeka la shughuli za kilimo kutokana na juhudi mbalimbali za kitaifa za kuleta mapinduzi ya kilimo.

Halikadhalika, wakulima hutumia viuatilifu feki bila kujua na dawa hizo ambazo hazina ubora huathiri afya za wakulima pamoja na mazao yao. Hata hivyo wakulima wengine hawafahamu kusoma jamii ya kiuatilifu, muda wa matumizi ya dawa hiyo na jinsi ya kuyatumia ni mtihani kwa kuwa hutegemea kuelezwa na wenzao.

Aidha, viuatilifu hivi ni tatizo kwa kuwa wakulima hawafahamu kuwa kitaalamu dawa au kemikali za kuua wadudu zipo katika madaraja mbalimbali kutegemeana na aina ya matumizi na kiwango cha sumu kilichopo.

Madaraja hayo yanahusu dawa mbalimbali kama za kuua wadudu, sumu za kuua fangasi (kuvu), zipo pia dawa za kuangamiza panya na wanyama wengine pamoja na zile za kuondoa madhara kwenye ardhi ama kwenye mimea (sanitizers)vitakasa.

### MAELEZO SAHIHI

Inavyoelekea huenda mambo haya kuhusu hali ya kemikali hayafahamiki ipasavyo kwa wakulima na mara nyingi wanaponunua hakuna mtu wa kuwapa maelekezo ya matumizi.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe kwenye baadhi ya maduka ya pembejeo Kariakoo jijini Dar es Salaam, unagundua kuwa wateja hununua bidhaa za ukulima hata bila kuuliza ushauri.

Mathalani, mkulima ananunua mbolea kilo kadhaa kwa ajili ya mahindi yenye wiki sita. Anapopimiwa hupokea na kuondoka.Anapoulizwa na gazeti hili anakwenda kuitumia namna gani anajibu kuwa anaiweka juu ya ardhi kwenye shina la mahindi.

Hata hivyo, anaposhauriwa kumuuliza muuzaji anapewa maelekezo tofauti kuwa mbolea aliyopewa ni 'CAN' hutumiwa kwenye mahindi ambayo yana wiki sita kama yake na anachotakiwa kufanya ni kuchimba kidogo kuzunguka mhindi urefu wa nchi sita au urefu wa kidole cha kati na kuweka mbolea kisha kuifukia.

Mkulima huyo anawakilisha wengi ambao hawafahamu hata namna ya kutumia pembejeo na matokeo yake ni kumwaga mbolea na kuiharibu pamoja na hasara pia husababisha madhara kwa bayoanuwai.

Wakulima na wafugaji wanatakiwa kuwa macho na kupata taarifa hasa kupunguza madhara. Kikubwa wanachotakiwa kufanya ni kuzuia matumizi ya kemikali hatarishi zinazotumika kwa muda mrefu bila kuharibika zikichafua hewa , vyanzo vya maji na hali ya ardhi.

Kemikali hizi ni kama vile DDT zamani iliyokuwa inatumiwa kutunza nafaka na nyakati hizi inatumiwa kuua vimelea vya malaria kwa kupulizia majumbani inaitwa dawa ya ukoko, kadhalika zipo dawa kama endrin chlordane na viambata kama dioxins na furans.

Pia zipo dawa kama thiodan ambazo hupulizwa kwenye pamba na kwa wakulima wa kahawa kulikuwa na dawa kama samathion iliyokuwa inatumika kwa wingi mkoani Kilimanjaro kuua mdudu aitwaye kimatira au kimatire aliyekuwa anafyonza majimaji kwenye matunda ya kahawa na kusababisha ziwe makapi.

Wakulima wengine bila kujali wanatumia kemikali kama josho (cattle dip) kuua wadudu hata kwenye mahindi au mboga wengine hata humwagilia vyooni au kwenye vichaka kufukuza nyoka . Japo kuna wanaoitmia kutibu upele mwilini mwao. Yote hayo ni matumizi hatarishi wanayokatazwa kwenye kemikali kama hizi ambazo huishi muda mrefu na kuathiri bayoanuia na kuleta maangamizo kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

### MADHARA KWA AFYA

Wataalamu wa kilimo pamoja na FAO wanaeleza kuwa baadhi ya magonjwa yanayotokana na athari za kemikali hatarishi za kilimo yanaweza kuwa ni pamoja na kuharibu mifumo ya mishipa ya fahamu ,saratani mbalimbali, magonjwa ya ngozi, kutetemeka mwili, maradhi ya figo pamoja na mapafu.

Kwa hiyo ni jukumu la mkulima ama mfanyakazi wa kemikali za kilimo na hasa madawa, kuwasiliana na wataalamu ili kujihami na kujilindaa na athari zinazotokana na sumu za viuatilifu.

Wakulima na wafugaji wanapokuwa mashambani ni vyema wakatambua kuwa kilimo kina madhara kama vile magonjwa ya kulemaa viungo kutokana kubeba mizigo mizito ,matatizo ya uti wa mgongo yanayosababishwa na kuinama muda mrefu na uhaba wa nyenzo za kisasa, aidha, matumzi yasiyokuwa salama ya pembejeo na kemikali huhatarisha afya na usalama shambani na kudhuru wazalishaji, walaji, bayoanuai na kutishia usalama wa maisha.





# Malori ya mizigo kupigwa marufuku

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imesema itapiga marufuku malori ya mzigo kuanzia tani 10, kuingia katikati mji mara baada ujenzi wa barabara ya mzunguko kukamilika.

Oktoba 23, mwaka 2019, Serikali ilitangaza kujengwa kwa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 112.3 baada ya kupata fedha Sh.Bilioni 494 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ambapo ujenzi utafanyika kwa miezi 36.

Akizungumzia mikakati ya Jiji hilo kujiepusha kukumbwa na foleni, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwekeza miradi mikubwa.

Alisema ujenzi huo utasaidia kuondoa uharibifu na msongamano wa malori hayo katikati ya Jiji hilo.

"Barabara hii ya mzunguko italizunguka jiji la Dodoma, magari makubwa ya mzigo kuanzia tani 10 hayataruhusiwa kuingia katika ya Mji," alisema.

Sambamba na hilo, Kunambi alisema Jiji limeanza usanifu wa ujenzi wa reli kilometa 100 ili kujiepusha na tatizo la foleni ya magari.

Alisema Dodoma inakuwa kwa kasi na kutokana na hali hiyo wameona kuanza mchakato wa kujenga reli.

Kunambi, alisema kuwa hivi sasa wameanza usanifu wa ujenzi huo ambao utalifanya Jiji hilo kutokuwa na foleni.

"Treni hiyo itakuwa kiunganishi katika maeneo ya mji wa kiserikali Mtumba, uwanja wa ndege Msalato pamoja na maeneo yote ya barabara za mzunguko (Ring road)," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa miradi yote ya kimkakati katika Jiji la Dodoma itakapokamilika itabadili kwa kiasi kikubwa muonekano na kuwa la kuvutia kuliko maeneo mengine nchini.

**Treni hiyo itakuwa kiunganishi katika maeneo ya mji wa kiserikali Mtumba, uwanja wa ndege Msalato pamoja na maeneo yote ya barabara za mzunguko (Ring road).**

# Askofu EAGT akemea mzaha katika corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la EAGT Dodoma, Evance Chande, amekemea baadhi ya watu ambao wanafanya mzaha kwenye ugonjwa wa corona na kuwataka kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali.

Aidha, amewaomba wanahabari kutoa elimu kwa wananchi waishio vijijini ili kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa huo.

Askofu Chande alitoa kauli hiyo jana, katika Ibada ya Jumatatu ya Pasaka iliyofanyika katika kanisa hilo Ipagala jijini hapa.

Alisema ugonjwa huo sio jambo la kulifanyia mzaha kwa kuwa ni la kidunia na limeangamiza watu wengi na kuathiri uchumi.

**Pia serikali iangalie namna bora ya kuwapatia huduma waliowekwa karantini ili wasitoke toke ovyo hadi watakapomaliza siku zao 14.**

Hata hivyo, alisema bado hakuna elimu ya kutosha hasa watu waishio vijijini, hivyo waandishi wanatakiwa kutumia nafasi yao kwa jamii kutoa elimu ya corona.

"Hapa mtaona kuwa baada ya serikali kutangaza kuwapo kwa ugonjwa huu, waandishi wa habari na vyombo vya habari vilijitahidi na vinaendelea kujitahidi kutangaza jambo ambalo limesababisha kila mmoja kujua kinachoendelea," alisema.

Alieleza kuwa vyombo vya habari kwa kutumia weledi wao utakuwa msaada mkubwa kwa jamii kwa kutoa elimu hata maeneo ya pembezoni.

Aliwashauri Watanzania kuhakikisha wanaweka vitakatisha mikono na maji yanayotiririka na sabuni ili kudhibiti maambukizi.

Kwa upande wake, Askofu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAM T), Kanda ya Kati, Julias Bundala, aliiomba serikali kuongeza ulinzi mipakani ili kukabiliana na watu ambao wanaingia nchini na ugonjwa huo.

"Pia serikali iangalie namna bora ya kuwapatia huduma waliowekwa karantini ili wasitoke toke ovyo hadi watakapomaliza siku zao 14," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa dini kuhakikisha wanafanya maombi yasiyokuwa na mzaha ili Mungu atoe ufumbuzi wa kukabili ugonjwa huo.



Wazoa taka kwenye makazi ya watu eneo la Kisasa jijini Dodoma, wakiendelea na kazi hiyo kwa kuweka kwenye gari la kubebea taka kama walivyokutwa hapo jana, magari hayo yamekuwa pia yakichangia kuharibu mazingira kwa kuangusha taka hizo barabarani yanapopita. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC Mahenge aiagiza Tarura kurejesha mawasiliano Zuzu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameuagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), kutengeneza njia mbadala ili kurudisha mawasiliano yaliyokatika katika Kata ya Zuzu jijini Dodoma.

Dk. Mahenge alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea eneo hilo baada ya barabara kujaa maji yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Alisema mawasiliano hayo yamekatika kati ya wakazi wa Zuzu na eneo la viwanda, hivyo ni vyema Tarura wakarejesha kwa kutengeneza njia mbadala ili kusitokee athari za kiuchumi.

"Muende mpendekeze barabara ya kuchepuka ambayo itatumiwa na wananchi ...kama ni viwanja kifanyike kitu gani, ni muhimu wananchi wasiwe locked (kufungiwa) ndani ya Jiji," alisema.

Alibainisha kuwa kuna viwanda hawawezi kutoka na hata likitokea tatizo kuwatoa itakuwa ngumu kutokana na hali ilivyo kwenye eneo hilo.

"Lazima kuwe na barabara ambayo watu wanaingia na kutoka na kufanya shughuli zao bila kikwazo," alisema.

Naye, Mratibu wa Tarura Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe, alisema wamepokea maelekezo ya mkuu huyo na watakaa na Jiji pamoja na wataalamu wa mipango miji ili kupata suluhisho la kudumu.

"Tunataka tupate njia mbadala ili ipitike wakati wote kama alivyoagiza Mkuu wa Mkoa," alisema.

Katika hatua nyingine, Wakazi wa Nkuhungu wameliomba Jiji la Dodoma kutengeneza barabara iliyopo eneo la Mfaume kutokana na kuharibiwa kwa kiwango kikubwa na mvua.





# Askofu Nyaisonga ataka bidii zaidi mapambano ya corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Mhashamu Gelvas Nyaisonga, amewataka Watanzania kuongeza bidii kwenye mapambano dhidi ya virusi vya corona ambavyo vimekwamisha baadhi ya shughuli za kijamii.

Nyaisonga ambaye pia ni Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya, aliyasema hayo juzi alipoongoza Ibada ya Pasaka katika Parokia ya Mwanjelwa jijini Mbeya ambapo alisema ugonjwa huo umeanza kuathiri hata uhuru wa watu kuabudu.

Alisema ugonjwa huo umekuwa ni tishio la kimwili na kiroho kwa binadamu, hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kukabiliana nao kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwamo kuhakikisha wananawa mikono kwa kutumia sabuni na maji yanayotiririka.

**Mbali na tahadhari walizozichukua kanisani hapo, lakini pia waliwaelekeza waumini wao kuchukua tahadhari hizo wakiwa nyumbani na kwenye maeneo yao ya kazi.**

Alisema ugonjwa huo unakwamisha shughuli za maendeleo kwa kuwa umesababisha watu wote kuelekeza nguvu na rasilimali nyingi kukabiliana nao badala ya kufanya shughuli zingine.

"Tukicheza na adui huyu tutapoteza hata huu uhuru wa kuabudu, kwa sasa mikusanyiko imekatazwa na tunakoelekea hata makanisa yatafungwa, hivyo hatutakuwa tena na huu uhuru tulionao," alisema Askofu Nyaisonga.

Aliwataka wazazi na walezi kuwalinda watoto wao dhidi ya ugonjwa huo kwa kuwazuia wasizurure mitaani kipindi hiki ambacho Serikali imezifunga shule na kutoa maelekezo kuwa watoto wakae nyumbani.

Mwenyekiti wa Parokia ya Mwanjelwa ambapo ndipo lilipo Kanisa na Hija la Bikra Maria wa Fatma, Augustino Kafukwa, alisema Kanisa hilo limechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo kuandaa maji na sabuni kwa ajili ya waumini kunawa kabla ya kuingia kanisani.

Alisema moja ya maelekezo ambayo waliwapatia waumini wa kanisa hilo ni kuepuka kugusana na kuepuka mikusanyiko ambayo inaweza ikasababisha watu kuwa katika hatari ya kuambukizwa virusi hivyo hatari.

Alisema mbali na tahadhari walizozichukua kanisani hapo, lakini pia waliwaelekeza waumini wao kuchukua tahadhari hizo wakiwa nyumbani na kwenye maeneo yao ya kazi.

Baadhi ya waumini wa Kanisa hilo waliohudhuria ibada hiyo, walisema elimu waliyopatiwa na viongozi wao itawasaidia kukabiliana na ugonjwa huo endapo kila mmoja atazingatia na kutekeleza maelekezo.

Alphonce Kidiga, alisema mahubiri ya Askofu Nyaisonga yalijikita zaidi katika kuhamasisha usafi wa mwili pamoja na mazingira, na kwamba maelekezo hayo yana maana kubwa kwa Watanzania.

Alisema usafi unaosisitizwa na viongozi mbalimbali wa dini na Serikali umesisitizwa pia kwenye vitabu vitakatifu, na kwamba usafi huo sio kwa ajili ya mapambano dhidi ya Corona pekee bali na magonjwa mengine.

## Sehemu za kustarehe kutofungwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

LICHA ya tishio la ugonjwa wa corona kuzidi kuongezeka nchini, Serikali mkoani Mbeya imesema, haina mpango wa kuzifunga sehemu za starehe zikiwamo baa kama sehemu ya kukabiliana na maambukizi.

Badala yake imewataka watu wanaoenda kustarehe kwenye maeneo hayo kuchukua tahadhari.

Akizungumza wakati wa kutoa elimu kwenye maeneo ya starehe jijini Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka watu wanaokwenda kwenye maeneo hayo kuepuka kusogeleana, huku akiwataka kuacha kudanganyana kuwa pombe ni dawa ya kuzuia ugonjwa huo.

Pia, aliwataka kuacha kuanzisha uhusiano wa kimapenzi kwenye maeneo ya starehe kwa maelezo kuwa wakifanya hivyo watajiweka kwenye hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo ambao ni ishio duniani.

"Tunaposikia kwamba ugonjwa wa corona upo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na maeneo mengine, tusifikiri kwamba Mbeya tupo salama, hatuna ukuta wa kuzuia usitukute, bali kila mmoja anatakiwa achukue tahadhari," alisema Chalamila na kuongeza:

"Utafanya mapenzi kwa kutumia kondomu ukikwepa Ukimwi, lakini corona haina kondomu, hivyo lazima tufuate maelekezo ya wataalamu wa afya yanayotolewa kila siku ili tuwe salama."

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwataka wamiliki wa maeneo ya starehe kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya kuhusu taratibu za uendeshaji wa maeneo hayo ili kuepuka kushughulikiwa.

Alisema mmiliki yeyote wa eneo la starehe ambaye atashindwa kuzingatia taratibu zilizowekwa, atafungiwa eneo lake pamoja na kuchukuliwa hatua za kisheria.



Fundi wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), akiunganisha umeme katika eneo la Forest jijini Mbeya, wiki iliyopita, baada ya kutokea hitilafu ya umeme iliyosababisha moto kuwaka na kuhatarisha nyumba zaidi ya 20 pamoja na maduka. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watano mbaroni tuhuma za kukutwa na noti bandia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu watano kwa tuhuma mbalimbali wakiwamo wawili ambao wamekamatwa na noti bandia za mataifa mbalimbali zikiwamo Dola za Marekani pamoja na vifaa vya kutengenezea noti hizo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakati wa msako wa Jeshi hilo uliofanyika maeneo mbalimbali ya mkoa huo wakati wa maandalizi ya sherehe za Pasaka.

Alisema katika tukio la kwanza, watu wawili ambao ni John Francis (22), mkazi wa wilaya ya Kyela na Peter Mwakamenya (37), mkazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi walikamatwa kwa nyakati tofauti Aprili 11, mwaka huu wakiwa na noti bandia.

Alisema Francis alikamatwa Mtaa wa Sokoni katika Kata ya Kyela kati saa 6:30 usiku akiwa na dola bandia tisa kila moja ikiwa na thamani ya dola 100 na noti bandia za Zambia kwacha 40 kila moja ikiwa na thamani ya kwacha 100.

Kamanda Matei alisema Mwakamenya alikamatwa na dola bandia mbili za kimarekani kila moja ikiwa na thamani ya dola 100 endapo zingekuwa halali, noti bandia za Tanzania ambazo saba ni za thamani ya Sh. 10,000 kila moja, mbili za Sh. 5,000 pamoja na kwacha za Zambia tatu kila moja ikiwa yenye thamani ya kwacha 100.

"Hawa wanajitengenezea hizi noti kisha wanaanza kuzisambaza, na wana vifaa ambavyo huwa wanavitumia kutengenezea noti hizi, sasa tunaendelea na taratibu mbalimbali za kuwafikisha mahakamani.

Katika tukio la pili, Matei alisema watu wawili ambao ni Kulwa Watson (42) na Steward Charles (25), wote wachimbaji wa dhahabu katika Mji wa Makongolosi wilayani Chunya, walikamatwa na dawa za kulevya aina ya bangi.

Alisema watuhumiwa ambao wote ni wakazi wa mji huo, walikamatwa Aprili 10, mwaka huu katika Kituo cha Mafuta cha Tanganyika kilichopo mjini hapo.

Alisema watuhumiwa ni wasambazaji na watumiaji wa dawa hizo kitu ambacho ni kinyume cha sheria za nchi na kwamba upelelezi unaendelea ili kuwabaini wenzao na kisha kuwafikisha mahakamani.

Kamanda Matei alilitaja tukio la mwisho kuwa ni la mtu mmoja ajulikanaye kwa jina la Zeze Charles (29), mkazi wa Bwawani wilayani Chunya akiwa na pikipiki ya wizi aina ya Sinorai yenye namba za usajili MC. 417 CAR.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Aprili 10, mwaka huu katika Mtaa wa Relini akiwa na pikipiki hiyo ambayo ina thamani ya Sh. milioni 2.2, na kwamba upelelezi unaendelea.



## Wizara Elimu kuanzisha masomo ya nyumbani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imejipanga kuanzisha vipindi vya masomo kwa wanafunzi wa shule za serikali na binafsi ili kuwasaidia wanafunzi hao kujifunza wakiwa nyumbani katika kipindi hiki dunia ikiwa katika janga la virusi vya corona.

Vipindi hivyo vinatarajiwa kurushwa wiki ijayo katika vyombo mbalimbali vya habari na Mitandao ya kijamii ambavyo vimesajiliwa na Wizara na Tume ya Utangazaji Zanzibar ili kuhakikisha wanafunzi hawasahau masomo yao.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, aliyasema hayo wakati akizindua mkakati wa elimu kwa Wamiliki wa Vyombo vya Habari Zanzibar.

Alisema zaidi ya vipindi 20 vimeshaandaliwa kwa wanafunzi wa msingi, zaidi ya vipindi 88 kwa wanafunzi wa maandalizi na zaidi ya vipindi 88 kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Simai, alisema vipindi hivyo vitakuwa na mwamko mkubwa kwa watoto kuvutiwa na kuacha kutumia mifumo ya kielimu iliyozoeleka ambayo itawawezesha wanafunzi kujifunza hata wakati yatakapomalizika maradhi hayo.

Alisema vipindi hivyo kwa kiasi kikubwa vitawasaidia wanafunzi hasa wa maandalizi na msingi kutosahau masomo badala ya kutumia muda mwingi kucheza.

Alisema, vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kuunganisha nguvu zao kuwasaidia watoto kupata elimu katika kipindi hiki na kila nchi zimefunga shule na vyuo vikuu ikiwamo Zanzibar kutokana na corona.

Naibu Waziri huyo aliitaka Tume ya Utangazaji kuhakikisha inalisimamia suala hilo ili kuona kila chombo kinarusha vipindi hivyo kwa maslahi ya watoto ambao ndio taifa la baadae.

"Lengo letu ni kuona tunafanya vipindi ambavyo vitasaidia kufikisha malengo ya watoto wetu katika kipindi hiki kigumu cha taifa letu tukiwa na mapambano ya ugonjwa huu," alisema Simai.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji wa Wizara hiyo, Abdullah Mzee Abdullah, alisema ni vyema vyombo vya habari vikatilia mkazo suala hilo ambalo litawasaidia watoto.

Naye, Katibu Mtendaji Tume ya Utangazaji Zanzibar, Omar Said, alisema ni jukumu la vyombo vya habari kuhakikisha vinatekeleza maagizo yote yanayotolewa na serikali na kuviomba kuhakikisha vinatekeleza jukumu hilo kwa upendo na uzalendo katika kulitumikia taifa lao kipindi hiki kwa kufuata sheria na kanuni zilizopo.

# Askofu Shao ashauri sera zikazie kilimo chakula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Agostino Shao, amesema ni vyema wakati huu wa ugonjwa wa corona sera za nchi zikazie kilimo cha mazao ya chakula na inapowezekana watu wawezeshwe.

Akizungumza katika Ibada ya Pasaka juzi, alisema ujumbe wa ufufuko wa Kristu ni agizo la kutafuta mbinu bayana za kupunguza umasikini unaowabana Watanzania wengi.

Alisema mbinu za kupunguza umasikini Tanzania ni kuwa na uongozi adilifu, sera safi zitakazosimamiwa vizuri.

Alisema ni vyema kukawa na utumiaji mzuri wa rasilimali za nchi na uzalendo wa raia kwa nchi yao kwa sababu ya corona.

**Mengi aliyoyaleta Kristu mfufuka ni matumaini ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi ili wapate ajira.**

Askofu Shao alisema habari za uchumi ulimwenguni sio nzuri, kuna mwanguko mkubwa wa uchumi kwa sababu ya corona.

"Ndugu zangu swali letu ni kupunguza umasikini Tanzania na si kumaliza, njia nyingi za kuzalisha zimefungwa na hivyo wengi kukosa ajira pamoja na changamoto ya corona bado watu wanahitaji mahitaji muhimu," alisema.

Alisema Zanzibar ambayo ni kisiwa ikiangalia sehemu kubwa ya uchumi ni utalii, kwa hali ilivyo huo ni uchumi unaotegemea uwezo wa watu wachache na wanaotaka faida kubwa.

Alisema Mungu amewabariki waja wake ukarimu mkubwa ikiwamo mvua nzuri hivyo kilimo cha mazao ya chakula na hasa matunda ya tropikali na mazao ya ukanda wa pwani kiwe kipaumbele cha nchi.

"Tukiwa na chakula kutoka shambani makali yatapungua, pale panapowezekana nyenzo zitolewe kwa kuboresha kilimo, tunaomba benki zetu zitengeneze mkopo nafuu na serikali iwe mdhamini," alisema Askofu Shao.

Alisema mengi aliyoyaleta Kristu mfufuka ni matumaini ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi ili wapate ajira.

Aliwataka kufahamu kuwa hali imebadilika bila ya mategemeo, hakuna budi nao wabadilike pia kutodharau kilimo na kuitumia fursa hiyo.



Baadhi ya wananchi wakiangalia eneo lililojaa maji Sebleni mjini Unguja, kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wauzaji gesi majumbani kukata leseni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAUZAJI wakubwa na wasambazaji wa gesi ya kupikia wametakiwa kukata leseni kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa ili kuhakikisha biashara hiyo inaendeshwa kwa misingi ya usalama na viwango vinavyokubalika.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Hassan Juma Amour, alisema, kanuni hiyo imeweka vigezo maalumu kwa waingizaji na wasambazaji wa nishati hiyo ikiwamo kuwa na sehemu maalumu ya kuhifadhi mitungi ambayo itakuwa mbali na makazi ya watu.

Alisema vigezo ni lazima sehemu inapouzwa mitungi hiyo iwe na mitambo iliyokaguliwa na Wakala wa Mizani na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ili kujua kuwa mitambo hiyo ipo salama kwa ajili ya kutia gesi katika mitungi.

Amour, alisema hiyo ni hatua ya pili ya kudhibiti sekta hiyo nchini ikiwamo hatua ya kwanza ya kuelimisha wadau jinsi ya kuendesha biashara hiyo kwa mujibu sheria na kanuni zao.

"Tayari tumeshakaa chini na waingizaji wakubwa, wasambazaji na wauzaji wa rejareja lengo ni kuwapa elimu na miongozo ya kuendesha biashara hii kwa misingi ya usalama na kuwafahamisha jinsi kanuni zinazovyoeleza usafirishaji na mambo mengine," alisema.

Alisema zoezi hilo baadae litahusisha wauzaji wa rejareja ili kuona kila mtu anakuwa na leseni iliyokuwa kisheria.

"Tumeona kwanza tuanze kwa hawa waingizaji wakubwa kwa kuwa wauzaji wa rejareja wapo wengi na wao watakuwa mabalozi wazuri kwa hao wanaowasambazia," alisema.

Alisema, hivi sasa soko la gesi ya kupikia hapa Zanzibar, limekuwa kwa kasi hivyo mamlaka imeona kunahitajika udhibiti na jambo hilo linahitaji kusimamiwa kwa nguvu zote kama inavyosimamia sekta ya mafuta.

Ofisa huyo alieleza kuwa, ZURA ina jukumu la kusimamia shughuli za nishati ikiwamo gesi ya kupikia majumbani ili kuona

# Shirika lawapa elimu ya corona watoto mitaani

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la 'Babawatoto Organization' katika kuadhimisha siku ya kimataifa ya mtoto anayeishi mtaani, limetoa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa virusi vya corona kwa watoto wa mitaani, ikiwa ni njia ya kulinda kundi hilo na majanga.

Siku ya kimataifa ya mtoto anayeishi na kufanya kazi mtaani huadhimiwa Aprili 12 kila mwaka, lakini mwaka huu kilele kitakuwa kesho.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Mgunga Mwamnyenyelwa, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kujenga ushawishi kwa wanajamii na serikali kuwekea mkazo zaidi suala la haki na ustawi wa watoto wakiwamo wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

"Shirika la Babawatoto linatekeleza mradi uitwao 'kizazi kipya' ambao unalenga kutetea haki kwa watoto na vijana wanaoishi na kufanya kazi mtaani, ikiwamo kutoa huduma za kibinadamu kama afya, kupima virusi vya Ukimwi, kuwapa chakula na elimu ya msingi na ufundi ili hatimaye wajitoe kwenye maisha ya mtaani," alisema Mgunga.

Alisema mradi huo ambao uko chini ya Pact Tanzania na Railway Children Africa (RCA) kwa ufadhili wa mashirika ya misaada ya USAID la Marekani na UKAID la Uingereza tangu mwaka 2017, umehudumia watoto 1,914 wasichana wakiwa 352 na wavulana 1,562.

Alisema ujumbe wa mwaka huu unaitaka jamii kutambua kwamba watoto wote wanastahili kujisikia kuwa salama hivyo jamii yote iwajibike, watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya vurugu na manyanyaso pasipo kujali wanatoka katika maisha ya aina gani.

Alisema jamii inapaswa kuchukua hatua zaidi katika kuwezesha ulinzi wa mtoto anayeishi mtaani kwani mara nyingi mtoto husahaulika.

**Jamii inapaswa kuchukua hatua zaidi katika kuwezesha ulinzi wa mtoto anayeishi mtaani kwani mara nyingi mtoto husahaulika.**


TASOTA

## TAARIFA KWA UMMA

14 April 2020

**Kwenda,**

**WATEJA WA JUMUIYA YA TASOTA**

Sera ya malipo ya safari wakati wa janga la virusi vya corona

Ugonjwa wa virusi vya corona kwa sasa umeshaathiri kila sehemu ya dunia. Tunawatakia kila la kheri na maombi kwa watu wote, pia kwa wote walio mstari wa mbele katika kutoa msaada wa kitabibu.

Sekta ya usafiri ni mojawapo ya eneo lililoathirika na ugonjwa huu.

Kwa niaba ya wanachama wa TASOTA Tanzania tunapenda kutoa taarifa kwa umma juu ya utaratibu kuhusu malipo na urudishaji wa gharama za tiketi za ndege kwa wakati huu.

Kama mnavyofahamu, mawakala wote wanapaswa kulipa IATA ndani ya siku 7 au 14 kwa mzunguko hapa nchini.

Kwa kipindi hiki cha janga la corona hakuna nafuu yoyote iliyotolewa na IATA au muda kurefushwa kuhusu muda wa malipo.

Kwa maana hiyo, mawakala wote watalazimika kuendelea kulipa gharama zinazohusika ndani ya siku hizo, vinginevyo watapoteza leseni zao za uendeshaji.

Katika kipindi hiki, tunawaomba wasafiri wote ambao wameshanunua au watanunua tiketi waelewe na kukubaliana na sera ya sasa na mzunguko wa malipo unaotolewa na mawakala wao.

Kila Shirika la ndege na wasambazaji wanautaratibu wao wa marejesho na ni vema wasafiri kuwasiliana na wakala kuhusu masharti yatayohusu safari.

Kama unahitaji marejesho, TASOTA inawataka wasafiri wote kulipia tiketi zao kikamilifu kulingana na masharti yaliyopo katika makubaliano na wakala wako.

Wanachama wetu pia watakurudishia pindi taratibu za marejesho yakikamilika na kupokelewa.

Tafadhari zingatia kwa kipindi hiki, kulingana na tatizo la corona na mawakala wote ulimwenguni kudai marejesho, IATA imeongeza muda wa marejesho, Sasa Marejesho yatafanyika kuanzia siku 60 hadi 90.

Huu ni wakati mgumu kwetu sote, na tunawomba wateja wote kuwa na uwelewa na kufuata masharti ya malipo na wakala wako.

*KAMATI TENDAJI TASOTA*


# Wasiojulikana walivyojeruhi mwanakijiji kwa panga


**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Kinyope, Kata ya Rutamba, Halmashauri ya Lindi/Mtama, Mkoani hapa,Yazidu Ally (31), amelazwa Kituo cha Afya Mandawa, akiuguza majeraha aliyoyapata kutokana na kujeruhiwa kichwani kwa panga.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Foka Dinya, alithibitisha kujeruhiwa kwa Yazidu, na kueleza alishambuliwa kichwani eneo la kichogoni, huku wahusika wa kitendo hicho wakimtelekeza kando ya barabara itokayo Milola kwenda Ngongo kisha kutokomea kusikojulikana.

"Jeshi la Polisi tunaendelea kuwasaka waliohusika na kitendo hicho ili sheria ichukue mkondo wake," alisema Foka.

Pia, alisema hali ya majeruhi huyo inaendelea vizuri kufuatia huduma ya matibabu.



Mwonekano wa mji wa Iringa, baada ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kutengua sheria ya wananchi wenye nyumba chakavu kutokarabati hadi wajenge ghorofa, ambapo sasa ukarabati unafanyika. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Serikali kuwapa waajiri msimamo kuhusu corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amesema serikali inatarajia kutoa msimamo wake utakaobainishwa kwa kila mwajiri ili kuzingatia miongozo ya pamoja ya ajira husususan kipindi hichi cha kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Kwa mujibu wa Mavunde, Waziri(Jenista Mhagama), alishatoa maelekezo kwa waajiri kitowaondoa wafanyakazi kiholela kwenye ajira bila kuzingatia utaratibu kwa kudai kuwa ni kutokana na janga la corona.

Mavunde alisema pamoja na maelekezo hayo, msimamo wa serikali utabainishwa ili kila mwaajiri azingatie.

"Ofisi ya Waziri Mkuu tunaendesha masuala yote kwa utatu, kwa maana ya wafanyakazi, waajiri na serikali, na tayari kikao cha pamoja kimeshakaa wiki iliyopita, tunasubiri maazimio na tutatoa maelekezo," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema pia watatoa maelekezo ya nini kifanyike na walikaa kwa pamoja na wamewashirikisha wote ili kujadili na kutoa ufafanuzi mzuri zaidi ili kila mtu aelewe msimamo wa serikali ni nini.

Kuhusu ajira kwa vijana, Mavunde alisema kwa sasa wanashirikiana na Wizara ya Kilimo ili vijana waweke mtazamo wao pia kujishughulisha na sekta ya kilimo.

"Ilionekana Kilimo ndio shughuli ya mwisho mtu kuifanya akikosa shughuli yeyote... sasa tumeona kama serikali kati ya maeneo ambayo yanaweza kutatua moja kwa moja matatizo ya ajira kwa vijana ni kushiriki kwenye sekta ya kilimo," alisema.

Alisema ndani ya miaka mitano mafanikio makubwa yameanza kuonekana, ambapo vijana wamebadili msimamo wao na kufanikiwa kupitia sekta hiyo.

HABARI KIMATAIFA

## Ndege ya Ufaransa yashambuliwa kwa risasi

**BRAZAVILLE,** Congo

NDEGE ya abiria ya Ufaransa iliyokuwa imewasili nchini Congo Brazaville kuwachukua raia wa Ufaransa kurejea nyumbani kufutia janga la virusi vya corona imeshambuliwa kwa risasi na maofisa wa usalama wa uwanja wa ndege wa Pointe-Noire.

Hata hivyo, usimamizi wa safari za ndege nchini Congo-Brazzaville na Shirika la ndege la Ufaransa la Air France, zimesema tukio hilo halikukusudiwa na sasa ndege nyingine inasubiriwa kuwasafirisha raia hao wa Ufaransa.

Ndege hiyo iliwasili Jumamosi ili kuwarudisha nyumbani raia wa Ufaransa wanaoishi nchini Congo.

Kulingana na vyanzo kadhaa, tukio hilo lilitokea Jumamosi jioni kati ya saa 9:30 usiku. na 9:50 saa za Congo-Brazzaville.

Hata hivyo, mamlaka ya uwanja wa ndege wa Pointe Noir imesema kuwa tukio hilo lilitokea kimakosa baada ya ofisa kutoka kikosi cha walinzi wa mipaka kujichanganya mwenyewe na kufyatua risasi bila kukusudia. **RFI**

## UNICEF yasema corona itaathiri watoto

**WASHINGTON,** Marekani

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), limesema janga la ugonjwa wa virusi vya corona linahatarisha mahitaji ya msingi ya watoto walio katika mazingira duni katika mataifa yanayoendelea na migogoro.

Mkurugenzi Mkuu wa UNICEF, Christian Schneider, aliliambia Shirika la habari la Ujerumani DPA kwamba ugonjwa huo ni tishio linalojidhihirisha wazi kwa idadi kubwa ya watoto.

Alisema fursa ya kuwanusuru watoto itawezekana endapo kutakuwapo na mpango utakaoratibiwa kimataifa katika kipindi hiki ambacho virusi vya corona vinasambaa katika makambi ya wakimbizi yenye idadi kubwa ya watu.

Schneider alisema hali kama hiyo pia itawakabili watoto wa ukanda wa Sahel na kusini mwa Afrika. **DW**

# Wazalisha mafuta wakubaliana kupunguza uzalishajiustria

**VIENNA,** Austria

WAZALISHAJI na washirika wa nchi zinazouza mafuta wamekubaliana kufikia makubaliano na kupunguza uzalishaji kote duniani kwa takriban asilimia 10 baada ya hitaji kupungua.

Hali hiyo imetokana na kuwapo kwa amri ya kusalia majumbani iliyotolewa na mataifa mengi duniani kama njia mojawapo ya kukabiliana na virusi vya corona.

Makubaliano hayo yaliyofikiwa Jumapili kupitia mkutano uliofanyika kwa njia ya video, ni ya kwanza kupunguza uzalishaji mkubwa wa mafuta ambayo hayajawahi kufikiwa siku za nyuma. Shirika la nchi zinazozalisha mafuta (OPEC) na washirika wake ikiwamo Urusi, lilitangaza mipango ya kufikia makubaliano hayo Aprili 9 ingawa Mexico haikuridhia ombi hilo.

OPEC bado haijatangaza rasmi makubaliano hayo lakini nchi husika zimethibitisha kuwa ziko tayari kwa mabadiliko.

Kile kilichothibitishwa hadi kufikia sasa, ni kwamba wazalishaji hao na washirika wake watapunguza uzalishaji wa mapipa milioni 9.7 kwa siku.

Mwanzoni mwa wiki, Barani Asia bei ya mafuta ilipanda kwa zaidi ya dola moja kwa pipa na kiwango cha mafuta ghafi cha asilimia 3.9 yakiuzwa kwa dola 32.71 kwa pipa, huku Marekani asilimia 6.1 ikiuzwa kwa dola 24.15 kwa pipa.

> **... lakini pia na wauzaji wakubwa duniani ambao ni Marekani pamoja na nchi zingine za G-20 ambazo zimekubali kuunga mkono makubaliano hayo kwa kupunguza uzalishaji.**

Hisa nchini Australia zilipanda kutoka asilimia 3.46 zikiongozwa na wauzaji wa mafuta lakini nchini Japani hisa za Nikkei 225 zilishuka kwa asilimia 1.35 kwasababu ya wasiwasi wa hitaji lililoshuka duniani kutokana na kusambaa kwa virusi vya corona.

"Makubaliano haya hayajawahi kufikiwa kabla kwasababu sio tu kati ya wazalishaji wa OPEC na washirika wake... lakini pia na wauzaji wakubwa duniani ambao ni Marekani pamoja na nchi zingine za G-20 ambazo zimekubali kuunga mkono makubaliano hayo kwa kupunguza uzalishaji," alisema Mkurugenzi wa utafiti wa mafuta katika kampuni ya Morningstar, Sandy Fielden.

Rais wa Marekani, Donald Trump na Waziri wa Nishati wa Kuwait, Dk. Khaled Ali Mohammed al-Fadhel waliandika ujumbe kwenye mtandao wa Twitter, huku Waziri wa Kazi Saudi Arabia na Shirika la habari la Urusi linalomilikiwa na serikali (TASS) wakithibitisha makubaliano hayo Jumapili.

"Kwa uwezo wa Mungu na uongozi wa busara, juhudi na mazungumzo endelevu tangu alfajiri Ijumaa, sasa tunatangaza kufikiwa kwa makubaliano ya kihistoria ya kupunguza uzalishaji kwa takriban mapipa milioni 10 ya mafuta kutoka kwa nchi za wazalishaji wa mafuta OPEC kuanzia Mei Mosi, 2020," aliandika Dk. al-Fadhel kwenye mtandao wa Twitter.

Hitaji la mafuta kote duniani linakadiriwa kupungua kwa theluthi moja wakati ambapo zaidi ya watu bilioni tatu wanafuata amri ya kusalia ndani kwasababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Kabla ya hapo, Machi, mwaka huu bei ya mafuta ilishuka vibaya baada ya nchi wazalishaji kushindwa kufikia makubaliano ya kupunguza uzalishaji.

Mazungumzo ya awali yalipata pigo baada ya Urusi na Saudi Arabia kushindwa kuafikiana, lakini Aprili 2, bei za mafuta ziliongezeka baada ya Rais Trump kuashiria kwamba anatarajia nchi hizo mbili kumaliza mgogoro wao. **BBC**



Abiria wakiwa ndani ya treni mjini Madrid jana. Baadhi ya kampuni zimeanza kufungua shughuli zao baada ya serikali kuwaruhusu. **PICHA: REUTERS**

# Chad yaendeleza operesheni dhidi ya wanajihadi

**N'DIJAMENA,** Chad

SERIKALI ya Chad imesema kuwa Jeshi lake litaendelea kushiriki katika juhudi za kikanda za kupambana dhidi ya makundi ya wanajihadi na ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa nchini Mali, baada ya kauli ya Rais Idriss Deby iliyozua sintofahamu.

Katika video iliyotolewa Ijumaa wiki iliyopita, Rais wa Chad alisema kuwa, wanajeshi wake wameuawa wakiwa katika shughuli ya kulinda amani katika Ziwa Chad na kwa eneo nzima la Saheli.

"Kuanzia leo hakuna mwanajeshi wa Chad atakayeshiriki katika operesheni za kijeshi nje ya Chad.

Maneno hayo yalitafsiriwa vibaya, alisema msemaji wa wizara ya mambo ya nje siku ya Jumapili.

"Chad haijawahi kutamka kuwa "itajiondoa katika kikosi cha mseto cha jeshi la kimataifa (FMM) kilichoundwa dhidi ya Boko Haram, wala kutoka kwa jeshi la pamoja la G5 Sahel au kutoka ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa nchini Mali".

Chad, ambayo jeshi lake linachukuliwa kuwa lenye ubora na nguvu zaidi katika ukanda huo, ni moja wa nchi muhimu katika mapambano dhidi ya makundi ya kijihadi huko Sahel na karibu na Ziwa Chad na ni mmoja ya wachangiaji wakuu katika ujumbe wa kudumisha amani nchini Mali. **RFI**

# ROMA WATAKA KUMBAKISHA MKHITARYAN KWA MKOPO




**LONDON,** England

MPANGO wa Arsenal kumuuza Henrikh Mkhitaryan kipindi cha majira ya joto unaonekana kukwama, huku AS Roma wakionyesha kutokuwa tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 22 zinazotakiwa na 'Washikabunduki' hao.

Mkhitaryan ametumia msimu huu kucheza kwa mkopo kule kwenye uwanja wa Olimpico baada ya kukosa namba katika dimba la Emirates chini ya kocha wa zamani, Unai Emery.

Kiungo huyo amekuwa akisumbuliwa na majeruhi wakati wake huko Serie A na ameanza katika mechi 13 za Ligi kwa klabu hiyo msimu huu.

Hata hivyo, akiwa dimbani amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho tatu.

Lakini kwa mujibu wa gazeti la Calciomercato la nchini Italia, ingawa Roma bado hawataki kutoa kiasi cha fedha kinachotakiwa kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Armenia, wameona nafasi kubwa ya kutaka tena kumtumia kwa mkopo kwa msimu mwingine.

Mkhitaryan bado hajui majaliwa yake, ingawa katika mahojiano yake ya hivi karibuni, alibainisha kwamba hajui hatima yake, lakini aliweka wazi kuwa amefiti zaidi kwenye mfumo wa uchezaji wa Roma kuliko alivyokuwa kule Arsenal chini ya Emery.

"Falsafa ya Emery ilikuwa tofauti na ya kocha wa Roma, Paolo Fonseca, lakini hapa najisikia vizuri zaidi kwa sababu tunacheza soka bora na nafikiri mimi ndio nafiti hapa," amesema mchezahi huyo mwenye umri wa miaka 31.

# Godin kutua Man United au Spurs

**MANCHESTER,** England

DIEGO Godin anatarajia kuondoka Inter Milan kipindi cha majira ya joto, huku akihusishwa na mpango wa kujiunga na timu za Ligi Kuu ya England.

Mlinzi huyo wa zamani wa Atletico Madrid, ambaye alijiunga na Inter kipindi cha majira ya joto mwaka 2019 kwa uhamisho huru, ameshindwa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza cha Antonio Conte msimu huu.

Kocha wa Inter amekuwa akimtumia zaidi Alessandro Bastoni na matokeo yake beki huyo mwenye umri wa miaka 34 anaweza kutua Manchester United au Tottenham katika miezi ya hivi karibuni, kwa mujibu wa gazeti la Tuttosport la nchini Italia.

Ripoti zimebainisha kwamba, mashetani wekundu hao wana nafasi kubwa zaidi ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay.

Hata hivyo, Spurs na kocha wake, Jose Mourinho wamekuwa wakimtolea macho Godin tangu atue pale kwenye dimba la San Siro.

Godin, ambaye alishinda taji la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, akiwa na Atletico mwaka 2014 na mara mbili alicheza fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, amecheza mechi 16 za Ligi Ku ya Italia, Serie A.

Amecheza mechi 136 kwa nchini yake tangu alipoanza kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 2005, na mwa sasa ni nahodha wa timu ya taifa.






# Rakitic: Mimi si gunia la viazi

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Ivan Rakitic amesema kwamba yeye si "gunia la viazi" wakati akitaka kuheshimiwa kipindi hiki kukiwa na shaka juu ya majaliwa yake kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Rakitic ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka Barca, huku akihusishwa kuwaniwa na klabu za Juventus, Inter, Manchester United na Paris Saint-Germain.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 majaliwa yake pale kwenye dimba la Camp Nou yanaonekana kufikia mwisho na mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia ameelezea hali yake.

"Mimi sio gunia la viazi," amesema Rakitic akiliambia gazeti la Mundo Deportivo, ambapo mahojiano yake yote yalichapishwa kwenye gazeti la jana Jumatatu.

"Nitaamua majaliwa yangu. Nataka kuwa sehemu nitakayopewa thamani yangu.

"Kama ni hana, nitafurahi, na kama sio, nitakuwa pale nitakapoamua."

Mkongwe Rakitic alijiunga na Barca kutoka kwa wapinzani wao, Sevilla mwaka 2014.

Tangu kutua hapo, Rakitic ameshinda mataji manne ya LaLiga na ligi ya mabingwa Ulaya.

# Chelsea sasa kumuuza Kante

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kwamba ipo tayari kumuuza kiungo wake, N'Golo Kante wakati wa dirisha linalokuja la kipindi cha majira ya joto.

Klabu za Real Madrid au Paris Saint-Germain zimeonesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo raia wa Ufaransa kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Kante, ambaye alijiunga na Chelsea mwaka 2016, amejitengenezea umaarufu wa kuwa mmoja wa viungo bora kabisa wakabaji kwenye soka la dunia na ameshinda EPL, Kombe la FA na Europa League akiwa na wakali hao wa Stamford Bridge.

Lakini, sasa Chelsea inafikiria kuachana na kiungo huyo baada ya Kocha Frank Lampard kuwaamini viungo wengine waliopo kwenye kikosi chake.

Taarifa kutoka Madrid zinadai Kocha Zinedine Zidane anataka kumsajili Kante, Paul Pogba pamoja na Mfaransa mwenzao Kylian Mbappe kwenda kufanya mambo katika kikosi hicho. PSG pia wanahitaji huduma ya Kante, ambaye mkataba wake umebakiza miaka mitatu huko Stamford Bridge.







# SANCHO KUCHAGUA KATI YA MAN UTD NA REAL

**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho "ataamua kati ya Manchester United na Real Madrid" baada ya nyota huyo wa England kuondoa uwezekano wa kujiunga na Chelsea.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 20, thamani yake ni pauni milioni 100 au zaidi, na anatarajiwa kuondoka Borussia Dortmund mara tu dirisha la usajili litakapofunguliwa kipindi cha majira ya joto baada ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Umekuwa ni msimu mzuri kwa Sancho ambaye amefunga mabao 17 na kutoa asisti 19 kwa Dortmund kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga na ligi ya mabingwa Ulaya na amekuwa bidhaa adimu Ulaya.

Na kwa mujibu wa gazeti la Hispania, Diario Madridista, Sancho sasa atachagua kati ya kwenda Old Trafford au kwenda uwanja wa Bernabeu baada ya kuondoa nafasi ya kutua Stamford Bridge.

Imeripotiwa kwamba United wanajiandaa kulipa fedha nyingi kwa ajili ya kumchukua mchezaji huyo wa zamani kutoka akademi ya City. Lakini Real Madrid hawawezi kuachwa kwenye mbio za usajili huo, kwani nao wameonesha nia ya kutaka kumsajili kwa muda mrefu.

Dortmund nao wangependa kumbakisha Sancho, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022.

# *Icardi hana maisha Inter Milan - Zanetti*

**MILAN,** Italia

MAKAMU Rais wa Inter Milan, Javier Zanetti amekubali kwamba, hafikirii kama Mauro Icardi ataendelea kubakia klabuni hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alipelekwa kwenda kucheza kwa mkopo kule Paris Saint-Germain kipindi cha majira kilichopita baada ya kutokuwa na uhusiano mzuri na kocha, Antonio Conte. Icardi alikuwa na wakati mzuri akicheza pale Parc des Princes ambako amefunga mabao 17 kwenye mechi 26 za Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Ripoti za hivi karibu zimebainisha kwamba, PSG wanataka kumpa mkataba wa kudumu Icardi kama akikubali kuondoka nchini Italia.

Hata hivyo, wakala wa Icardi ambaye ni mke wake, Wanda Nara, ameripotiwa kuiambia PSG kwamba wanafikiria kurudi nchini Italia katika klabu yake ya zamani ya Inter.

Lakini wakati alipoulizwa kuhusu uwezekano huo, Zanetti haoni kama hilo litawezekana.

"Sijui, sidhani kama hilo litatokea," amesema Zanetti akiiambia ESPN.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL, CHELSEA ZAITIWA COUTINHO

Mimi ni shabiki wa Gunners lakini sijaribu kumlazimisha mchezaji yeyote...

**LONDON,** England

PHILIPPE Coutinho angependa kurudi Ligi Kuu England wakati huu Arsenal na Chelsea zikihusishwa, kwa mujibu wa wakala wake, ingawa bado kuna uwezekano mkubwa wa mustakabali wake wa baadaye.

**Nyota wa kimataifa wa Brazil, Coutinho kwa sasa yupo Bayern Munich kwa mkopo akitokea Barcelona, lakini mabingwa hao wa Bundesliga hawatarajiwi kuufanya mkataba wake huo kuwa wa kudumu.**

Na wakati Barca ikitarajiwa kutaka kumuuza kiungo huyo, ambaye alijiunga na klabu hiyo akitokea Liverpool kwa dili lililoigharimu euro milioni 160 Januari mwaka jana, inaaminika kurudi England kunaweza kuwa chaguo bora zaidi kwake.

Chelsea na Arsenal zimekuwa zikihusishwa na kutaka kutoa ofa, na mwishowe alisema kuwa chaguo la kweli kama Kia Joorabchian, wakala wa Coutinho, ni shabiki wa 'Gunners'.

Hata hivyo, Joorabchian aliiambia Sky Sports News: "Ukweli mimi ni shabiki wa Arsenal si siri.

"Sina upendeleo wowote wapi wachezaji wanakwenda. Sijaribu kumlazimisha yeyote kutoka klabu moja kwenda nyingine. Kila kitu ni uwezekano.

"Baada ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya alicheza England [wakati Bayern Munich ikiichapa Chelsea 3-0], tulikuwa na muda mrefu wa 'kuchati' kuhusu hilo.

"Ligi Kuu England ni kitu ambacho mara zote anafurahia kucheza hapo, na ninapenda acheze hapo, na pengine angependa kurudi na kucheza hapo. "Swali ni kwamba itakuwaje hali ya kifedha kwa klabu zote, ikiwamo Barcelona na klabu zote za Ligi Kuu mwishoni mwa janga la kidunia la corona."

Joorabchian pia ni wakala wa kiungo mshambuliaji wa Chelsea, Willian, ambaye anatajwa kutaka kuondoka mwishoni mwa msimu baada ya mazungumzo ya mkataba mpya kuvunjika kutokana karantini ya mlipuko wa virusi vya corona.

Hata hivyo, wakala huyo amesisitiza hajazungumza bado na mteja wake hivi karibuni kuhusu uwezekano wa uhamisho kufuatia mpasuko huo uliosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona.

"Kuna uvumi mwingi, lakini naweza kukuelezea kwa dhati hatujazungumza juu ya uhamisho au kitu chochote kama hicho," alisema.

"Hakuna yeyote mwenye hisia sahihi. Sio sisi au upande mwingine tuna hisia ya kujadili jambo wakati mambo mengi yanatokea ulimwenguni kote ambayo ni muhimu sana."

Joorabchian alikuwa na hamu ya kutoa pole kwa wahudumu wa afya huko Uingereza, ambapo watu 65,000 walithibitishwa kuambukizwa virusi vya corona huku vifo vikiwa 8,000 kabla ya jana idadi ya waliokufa kupanda hadi 9,594 na walioambukizwa kufikia 66,330.

## ZISIKUPITE

### SANCHO AICHOMOLEA CHELSEA

WINGA wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 20, havutiwi kujiunga na Chelsea, hivyo kuiacha Manchester United katika nafasi nzuri kuinasa saini yake, ingawa Real bado nayo inamulika. ***(Diario Madridista, in Spanish)***

### BARCELONA KWA NDOMBELE

BARCELONA inapewa nafasi kubwa ya kumsajili kiungo wa Tottenham, Tanguy Ndombele, 23. ***(Star)***

### MADRID YAMFUATA RODRIGUEZ

EVERTON imejiunga katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez. Manchester United na Juventus pia zinavutiwa na nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ***(Express)***

### CHELSEA KUMRUDIA MERTENS

CHELSEA itatoa ofa ya pili kwa kiungo wa Napoli na Ubelgiji, Dries Mertens, 32. 'Blues' walitoa ofa kwa mchezaji huyo katika dirisha la Januari ambayo ilikataliwa, lakini Mertens bado hajasaini mkataba mpya na miamba hiyo ya Italia. ***(Gazetto dello Sport, in Italian)***

### MKHITARYAN NJIAPANDA ROMA

ROMA haipo tayari kufika dau la pauni milioni 22 zinazohitajiwa na Arsenal ili kumwachia kiungo Henrikh Mkhitaryan. Muarmenia huyo mwenye umri wa miaka 31, anaichezea klabu hiyo ya Italia kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu. ***(Calciomercato, via Star)***

### MARTINEZ KUMFUATA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez, 22, anaweza kujiunga na mchezaji mwenzake raia wa Argentina, Lionel Messi katika kikosi cha Barcelona, amesema wakala wake. Manchester City hivi karibuni ilipewa nafasi ya kumsajili. ***(Fox Sports Mexico, in Spanish)***

### GODIN ATAKA KUTUA EPL

BEKI wa Inter Milan na Uruguay, Diego Godin anaweza kutua Ligi Kuu England majira ya joto. Manchester United na Tottenham zinavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34. ***(Tuttosport, in Italian)***

### SPURS HAIKUMTAKA WILLIAN

MWENYEKITI Tottenham, Daniel Levy, angeweza kuzuia usajili wowote kwa kiungo mshambuliaji wa Chelsea, Willian, amesema beki wa zamani wa England, Danny Mills. Mbrazil huyo, 31, hivi karibuni alikataa ofa ya kujiunga na Spurs mwaka 2013. ***(Football Insider)***

### S'AMPTON, RALPH WAKUBALIANA

KOCHA wa Southampton, Ralph Hasenhuttl, amekubaliana kikanuni dili la kuendelea kubaki katika klabu hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu. ***(Sun)***

### ARSENAL KUOKOA MABILIONI

ARSENAL inajaribu kuokoa pauni milioni 25 kwa kuwakata wachezaji mishahara kama haitafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Telegraph)***

### RICE KUMFUATA MOUNT

KIUNGO wa West Ham na England, Declan Rice amesema angependa kwa mara nyingine kucheza pembeni ya kiungo wa Chelsea, Mason Mount. Wawili hao kila mmoja ana miaka 21, walicheza katika akademi ya Chelsea. ***(Copa90)***

## HABARI MICHEZO

## Dulla Mbabe ageukia Bajaji

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU majaliwa ya kuanza tena kwa shughuli za michezo baada ya kusimama kwa kipindi cha mwezi mmoja ikitarajiwa kujulikana Ijumaa wiki hii, bondia maarufu nchini, Abdallah Pazi 'Dulla Mbabe', ameelekeza nguvu zake katika mazoezi binafsi sambamba na kusimamia biashara yake ya bajaj na bodaboda.

Machi 17, mwaka huu, serikali ilisitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo za michezo kwa kipindi cha mwezi mmoja kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).



Hata hivyo, hatma ya kurejea tena kwa michezo nchini ama la inatarajiwa kujulikana Ijumaa wiki hii siku ambayo zuio hilo la mwezi mmoja lililotolewa na serikali litamalizika.

Lakini kwa bondia Dulla Mbabe yeye hakuwa na muda wa kupoteza kama ilivyo kwa baadhi ya wachezaji ambao wameripotiwa kujikita katika kula 'bata' (starehe) na badala yake amemwambia mwandishi wetu wiki iliyopita kuwa, kwa kipindi hiki ambacho serikali imezuia shughuli zote za michezo nchini yeye amekuwa 'bize' katika mazoezi binafsi pamoja na kusimamia biashara zake za bajaji na bodadoda.

"Nimepata muda zaidi wa kufanya mazoezi binafsi ili kujiweka fiti katika kipindi hiki lakini pia najishughulisha na kusimamia biashara zangu za bajaji na bodaboda," alisema bondia huyo huku akiendelea kujifua.

## Simba yamtoa udenda Odhiambo

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya umri kumtupa mkono, kiungo mnyumbulifu wa zamani wa Simba, Mkenya Moses Odhiambo, amesema ushindani wa namba uliopo katika kikosi hicho kinachonolewa na Mbelgiji Sven Vandenbroeck, unamtamanisha kuwa miongoni mwa jeshi hilo.

Odhiambo anayeichezea Nairobi Stima FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Kenya, jana aliliambia Nipashe kwa njia ya simu kutoka Nairobi, Kenya kuwa, Simba ya sasa inamvutia sana na anatamani tena kuichezea.

Odhiambo, 34, aliitumikia Simba mwaka 2007 kabla ya kutimkia APR ya Rwanda na kisha msimu wa 2009–2010 kurejea Ligi Kuu Bara na kuitumikia Yanga.

"Nijiamini kwa kiasi kikubwa naweza kurejea na kupambana kama wakinihitaji, mkataba wangu unamalizika Juni," alisema Odhiambo.

# HITIMANA AJIWEKA SOKONI RASMI, NAMUNGO YAHAHA

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Klabu ya Namungo ukiendelea kusubiri hadi mwishoni mwa msimu kujua hatma ya Kocha wao Mkuu, Mnyarwanda Thierry Hitimana, mwalimu huyo amejiweka sokoni baada ya kueleza yupo tayari kuinoa timu yoyote itakayofikia makubaliano naye.

Akizungumza na mwandishi wetu, Hitimana alisema mkataba wake na Namungo unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu na hadi sasa hawajafanya mazungumzo na klabu hiyo, hivyo anachoangalia kwake ni maslahi endapo itajitokeza klabu inayomhitaji na kukubaliana.

Alisema: "Nipo tayari kuifundisha timu yoyote, mkataba wangu unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu, kwa sasa nipo huru kuzungumza na klabu yoyote, lakini pia kama Namungo watanipa maslahi mazuri nitaendelea kuifundisha.

**"Siwezi kusaini mkataba mpya Namungo kwa mshahara huu wa sasa, hivyo wakiniongeza na tukafikia makubaliano sina tatizo."**

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alipolizwa kuhusu hatma ya kocha huyo, alisema walishaanza mazungumzo ya kumuongezea mkataba mpya lakini aliwataka kusubiri hadi msimu utakapomalizika.

"Hatuna mpango wa kubadilisha kocha, bado tuna mipango naye, tulikutana naye na alituambia hadi ligi itakapomalizika ndio ataongeza mkataba, hivyo hatima ya kubaki itakuwa mikononi mwake.

"Alituambia tusubiri, hivyo kama akikubali hatutasita kumpa mkataba hata wa miaka mitatu ama minne, kwa kuwa tulimpa malengo yetu ya kumaliza nafasi 10 za juu Ligi Kuu na ameyafikia na zaidi, hivyo bado tunamhitaji," alisema Zidadu.

Hadi Ligi Kuu inasimama kwa kipindi cha mwezi mmoja kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), Namungo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo ikiwa na pointi 50 baada ya kushuka dimbani mara 28 mechi sawa na Simba iliyopo kileleni na alama zake 71, ikifuatiwa na Azam FC pointi 54 na kisha Yanga yenye alama 51 lakini ikiwa nyuma mchezo mmoja.

**KITAELEWEKA...**



Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, akiwa na wasaidizi wake, Selemani Matola (kulia) na Kocha wa Makipa, Muharami Mohamed (katikati), katika mazoezi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, kabla ya Ligi Kuu kusimama kwa mwezi mmoja kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. Juzi kocha huyo alieleza kuvutiwa na ushirikiano mkubwa kutoka kwa wasaidizi wake hao. **PICHA: SIMBA**

# *Simba, Yanga zamtesa Malale*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, amesema Simba, Yanga na Azam FC ndizo zinazompa wakati mgumu kutokana na taarifa zinazozihusisha na baadhi ya wachezaji wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema mipango yake ya msimu ujao ni kutofanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake na kutaka kuongeza wachezaji wawili endapo nyota waliopo sasa wataendelea kuitumikia timu hiyo.

Alisema tayari kuna taarifa ya baadhi ya wachezaji wake kutakiwa na timu hizo hali inayompa wakati ngumu wa kukabidhi ripoti ya usajili kutokana na kuhitaji kusubiri muda ili kuona nyota watakaoondoka.

"Ukiangalia kikosi changu kipo vizuri, hivyo kama nitabaki nao wote basi nitafanya usajili katika nafasi chache kwa kusajili wawili, ila kwa sasa sitaweza kwa sababu nahofia wengine kuondoka kwa kusajiliwa na timu nyingine," alisema Malale.

Alisema anatarajia baada ya Ligi Kuu kumalizika atakutana na viongozi wake kwa ajili ya kumpa mikakati yake ya usajili na kuona nafasi zipi anahitaji kufanyiwa kazi kumpa mchezaji sahihi atakayeisaidia timu yao kwa msimu ujao.

"Pia nitaangalia vijana wetu wa Timu B, kuna wachezaji nimewaona nahitaji kuwapandisha, hivyo nitatumia michuano ya vijana kujiridhisha kwa kutazama viwango vyao," alisema Malale aliyeridhi mikoba ya Selemani Matola ambaye ameajiriwa Simba kama kocha msaidizi.

# Michezo

Jumanne Aprili 14, 2020

Nipashe




Arsenal, Chelsea zaitiwa Coutinho UKURASA 22

NJOONI MEZANI...



Kiungo wa Simba, Mzambia Clatous Chama (kulia), akiwa mazoezini na mchezaji mwenzake, mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere. Yanga inahusishwa na kuhitaji huduma ya Chama kwa ajili ya msimu ujao. **PICHA: MAKTABA**

## Ligi Kuu kurejea shida kwa timu

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU majaliwa ya kurejea kwa Ligi Kuu Bara yakitarajiwa kujulikana Ijumaa wiki hii siku ambayo zuio la kufanyika shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ikiwamo michezo, litamalizika, baadhi ya klabu zinaona kurejea kwa ligi hiyo kutakuwa shida kwao kuweza kuepuka janga la kushuka daraja.

Machi 17, mwaka huu serikali ilitangaza kusimama kwa ligi hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) wakati huo kukiwa na mgonjwa mmoja, hata hivyo wakati zuio hilo la mwezi mmoja likitarajiwa kumalizika Ijumaa wiki hii, hapa nchini kwa sasa watu waliobainika kuwa na maambukizi ya virusi hivyo ni 49, saba kati yao wakipona na kuruhusiwa kurejea nyumbani huku vifo vikiwa vitatu.

Kwa upande wa Alliance FC iliyopo nafasi ya 18 ikiwa na pointi 29 baada ya michezo 29, mmiliki wa klabu hiyo, James Bwire, alimwambia mwandishi wetu kuwa licha ya kuamini ligi hiyo ikirejea wanaweza kupigana na kuepuka kushuka daraja, lakini ikifutwa kwa msimu huu itakuwa jambo jema zaidi kwao.

"Ligi ikifutwa itakuwa jambo jema, lakini tunaamini bado tunaweza kupigana na kubaki Ligi Kuu msimu ujao kama ikirejea tena," alisema Bwire.

Kwa upande wa Kocha wa Coastal Union ya Tanga, Juma Mgunda, ambaye timu yake ipo nafasi ya tano ikiwa na alama 46 baada ya michezo 28, alisema bado ni mapema kusema lolote kuhusu ligi hiyo ifutwe ama iendelee.

"Afya ya wachezaji ndiyo kitu cha muhimu kwanza, tusubiri tamko la serikali baada ya zuio la mwezi mmoja kumalizika ndipo tunaweza kutoa maoni kuhusu ligi iendelee ama ifutwe," alisema Mgunda ambaye ameitengeneza Coastal kuwa timu ya ushindani mkubwa msimu huu.

# Yanga yaitiwa Chama Simba

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Lakini yabainika inazunguka mbuyu ikitaka kumalizana na TP Mazembe imsajili Kanda, yaambiwa...

WAKATI kiungo 'mnyumbulifu' wa Simba, Mzambia Clatous Chama, akiendelea kugonga vichwa vya habari kutokana na kuhusishwa na Yanga, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi hao, umewaambia "njooni mezani" tuzungumze.

**Kwa wiki kadhaa sasa, Yanga imekuwa ikihusishwa na kuhitaji saini ya Chama aliyejiunga na Simba mwaka 2018 na kusaini mkataba wa miaka miwili akitokea Lusaka Dynamos ya Zambia kabla ya mwaka jana kuongeza mingine miwili.**

Hata hivyo, tetesi za kumhusisha Chama na Yanga ziliibuka baada ya taarifa za chini kwa chini kuwa amegoma kuongeza mkataba na klabu hiyo, huku vyanzo hivyo vya habari vikisahau kuwa Mzambia huyo mwaka jana alisaini mkataba mpya wa miaka miwili.

Akisaini mkataba huo Juni 26, mwaka jana, taarifa ya Simba iliyolifikia Nipashe, ilieleza:"Mfungaji wa magoli ya mwisho ambayo yalitupeleka kwenye hatua ya makundi na robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Clatous Chota Chama (Triple C) bado yupo sana Msimbazi. Mwamba wa Lusaka ataendelea kuwa sehemu ya kikosi cha mabingwa baada ya kusaini mkataba mpya wa miaka miwili."

Hata hivyo, Simba imeiambia Yanga wanakaribishwa mezani kuzungumza dili la kumsajili mchezaji huyo kama inahitaji huduma yake. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, amesema kwenye mpira lazima biashara ifanyike na kwamba kama Yanga inamhitaji Chama wafuate taratibu za kuvunja mkataba wake wa miaka miwili uliobaki.

Senzo ameeleza kuwa kuvunja mkataba wa Chama si chini ya dola 350,000 za Marekani sawa na Sh. milioni 807.9 za Tanzania kwa sasa.

Hata hivyo, chanzo chetu kutoka ndani ya Yanga kimelieleza Nipashe kuwa, klabu hiyo inatambua kuwa Chama bado ana mkataba na Simba, lakini inachofanya kwa sasa ni kuchokoza tu kwani mchezaji wanayemtaka ni kiungo Mkongomani Deo Kanda anayeichezea klabu hiyo kwa mkopo kutoka TP Mazembe ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

"Tunajua wazi Simba haiwezi kutuuzia Chama, lakini kinachoendelea kwa sasa ni mazungumzo ya chini kwa chini na TP Mazembe ili kumnasa Kanda anayeichezea Simba kwa mkopo," kilieleza chanzo chetu.

Kanda amekuwa msaada mkubwa kwa Simba msimu huu baada ya kuiwezesha kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 71, wakati huu ligi hiyo ikiwa imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Licha ya Kanda kuwa majeruhi na kukosa mechi nyingi za mzunguko wa pili, katika mabao 63 Simba iliyofunga Ligi Kuu kutokana na mechi 28 ilizocheza hadi sasa, sita yamefungwa na Kanda ambaye wakati anatua Msimbazi mashabiki wa Yanga walikuwa wakiwabeza watani zao kuwa winga huyo si lolote kwa kuwa TP Mazembe haiwezi kumtoa mchezaji mzuri.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >